



# Nipashe

Jumatatu Septemba 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581437

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


**RIPOTI YA UCHUNGUZI** Vikundi hewa vilivyoishtua serikali ulaji wa mabilioni UKURASA 4



**BIL. 1/-** zatengwa ufadhili wanafunzi wa vyuo vikuu UKURASA 18




**ADAIWA** kumuua hawara wa binti yake kwa sumu UKURASA 18

# Kero kibao zatua Ikulu

Rais Samia ashtukia viongozi; aonya mila zinazochochea mimba utotoni... Ukurasa wa 2




Wananchi wa Masasi wakiwa kwenye shamrashamra za kumpokea Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Bomani, mkoani Mtwara jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 11


Nipashe
Spotika
SABABU 5 KWA NINI MESSI ATAMSHINDA HAALAND MBIO BALLON D'OR 2023

UKURASA WA 18

## WAWILI WAFA MGODINI WAKICHIMBA DHAHABU

WATU wawili wamefariki dunia wakati wakichimba madini katika mgodi uliofungwa wa Kanegere wilayani Mbogwe baada ya kuangukiwa na kifusi cha mchanga.

UKURASA WA 24

## SINGIDA FG YAIKAMUA FUTURE FC SHIRIKISHO

## 'Polisi Jamii ifutwe, tuwe na idara ya vibali vya kunyonga'

UKURASA 5

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

## Kibatala adai askari polisi amejifanya dada wa kazi

UKURASA 7

**MICHEZO** SIMBA, YANGA SC CAF HAIJAISHA MPAKA IISHE UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Rais Samia Suluhu Hassan akivuta kitambaa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe pamoja Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, kuashiria uzinduzi wa ghala na miundombinu ambatanishi ya mradi wa kudhibiti sumukuvu (TANIPAC), Nanyumbu mkoani Mtwara jana. **PICHA: IKULU**

# Kero kibao zatua Ikulu

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameshtushwa na Ikulu kuwa inapokea kero nyingi za wananchi moja kwa moja, zikiwamo toka vijijini.

Amesema hali hiyo aliyoitaja haipendekezi, inatoa ishara ya kutowajibika kwa watendaji ngazi zote kuanzia kitongoji au mtaa wanaotakiwa kufanya kazi hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Rais amewataka viongozi wa ngazi zote kuanzia ngazi ya mtaa hadi mkoa kutembelea wananchi katika maeneo yao ili kusikiliza na kutatua kero. Atakayekaidi, serikali haitomvumilia.

Rais Samia aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi wa Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara na Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi na kuongeza kuwa serikali imejizatiti kutatua kero za wananchi.

"Niombe sana, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) simamieni hilo, serikali hii mmeiweka ninyi.

Sasa mkijifanya wadogo na kufanya watendaji kuwa wakubwa, mnakosea! Wasimamieni watendaji warudi wawasimamie wananchi," aliagiza.

Akizungumza na wananchi wa Liwale, Rais alionesha kusikitishwa na baadhi ya wazazi kutopeleka watoto wao shuleni wakati serikali inaboresha elimu kwa kujenga shule na kuondoa ada.

"Niwasihi sana, sana, sana, ukombozi wa Liwale hii ni kupeleka watoto wetu shuleni. Watoto wa kiume na watoto wa kike waacheni wakasome, waende shuleni.

"Tunatoa fedha nyingi tukimaliza mitihani darasa la saba kwenda kidato cha kwanza tunafanya kusakana, watoto mnawaficha mnawapangia kazi nyingine, wengine mnawaozesha mapema," alionya.

Rais Samia alisema serikali kupitia mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora kwa Vijana (BBT) imejizatiti kutoa mafunzo kwa vijana mkoani Lindi ya kutumia rasilimali zilizopo ikiwamo ufugaji wa nyuki na kuvuna asali bora, na kuwatafutia masoko ili kujiinua kiuchumi.

Alisema mradi huo pia utatoa mafunzo ya kilimo ikiwamo korosho, ufuta, mbaazi na alizeti ili watumie vizuri utajiri wa ardhi waliojaaliwa kutanua shughuli za kilimo.

Kuhusu changamoto za wanyama waharibifu, Rais aliwahakikishia kuwa watakwenda kukaa katika ngazi ya kitaifa ili kuchukua hatua za haraka kukabiliana na wanyama hao, wakiwamo ndovu.

Alisema serikali inaendelea kuboresha barabara wilayani humo ikiwamo ya Nangurukulu kwenda Liwale - kipande cha kilometa 230. Kwa sasa wametenga bajeti ya kujenga kilometa 72 na kila mwaka wataongeza fedha hadi itakapokamilika.

Kipande hicho cha barabara hiyo ya vumbi kimekuwa kikwazo kikubwa cha usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Liwale.

Kipindi cha mvua magari yamekuwa yakikwama njiani. Hufikia hatua mabasi na malori ya mizigo kulazimika kutopitia njia hiyo, madereva wake wakilazimika kupitia mjini Lindi-Nachingwea ndipo waingie Liwale.

Ni kero ya muda mrefu ambayo imekuwapo tangu kuanzishwa kwa wilaya hiyo miaka 48 iliyopita baada ya kumegwa kutoka Nachingwea kutokana na ukubwa wa Wilaya ya Nachingwea.

Raia pia aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti katika misitu ili kuendelea kuhifadhi ikolojia ya nchi isiathirike zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema wilaya hiyo ina rasilimali za asili nyingi ikiwamo misitu yenye miti ya asili inayotoa mbao ikiwamo mninga ambazo kama zikitumiwa kwa njia endelevu zitanyanyua wakazi wa maeneo hayo, hivyo serikali inaangalia Mkoa wa Lindi kwa jicho la pekee.

Alielekeza wananchi kuhakikisha wanapokata miti katika misitu hiyo kwa ajili ya biashara na shughuli za kijamii, wahakikishe wanapanda mingine kwa kuwa bila kufanya hivyo, miti yote itakwisha na misitu itabaki mitupu.


PUBLICATION SUMMONS
IN THE DISTRICT COURT OF
BUKOBA AT BUKOBA
CRIMINAL APPEAL NO. 12/2023
Arising from the Judgement of Bukoba Primary Court at Bukoba in Criminal Case No. 176 of 2023 delivered on the 08/06/2023 Before Hon. Z.R. Nyahende.
SOSPETER BUKAGIRE ……APPELLANT
VERSUS
EMMANUEL NGAS…..1st. RESPONDENT
ELGIVA CLEVA ……. 2nd. RESPONDENT
NOTICE OF HEARING
TO: ELGIVA CLEVA
TAKE NOTICE that mentioned case has been set down for Hearing on the 22 day of SEPTEMBER, 2023 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. F.A. KAIJAGE – SRM. Your presence is therefore required on the date and the time indicated.
Given under my hand and the seal of the court this 12 day of SEPTEMBER, 2023
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA


# ...Aonya kukumbatia mila zinazochochea mimba utotoni

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wananchi wa mikoa ya kusini kuacha utamaduni wa kutumia fedha za mavuno katika kutekeleza mila na desturi za kuwacheza mabinti wakiwa na umri mdogo, hivyo kuchangia mimba za utotoni.

Alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na wananchi wa Masasi katika Uwanja wa Bomani, Halmashauri ya Mji Masasi, ikiwa ni sehemu ya ziara yake katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Ni baada ya wananchi wa maeneo mbalimbali alimopita kumwomba awajengee mabweni kwa ajili ya wasichana ili kupunguza mimba za utotoni ambazo wanaona zimekithiri.

Alisema amepata taarifa kuwa mimba za utotoni zinaongezeka baada ya mavuno, kipindi ambacho wazazi hutumia fedha za mauzo ya mazao ya biashara kuwacheza watoto wao, hivyo kuwapo mabweni hakutoweza kuondoa tatizo hilo kama wazazi wako tayari kutumia vipato vyao kwenye mambo yasiyo na tija.

"Mambo ya kuwacheza wasichana wakiwa wadogo, kisha unampa rukhsa 'umeshachezwa nenda', tuyaache. Haya hayawajengei mazingira mazuri wasichana wetu.

"Wachezeni wakiwa na umri wa kujua wamechezwa na wameyaelewa nayo (mafunzo kwenye kuchezwa)," Rais Samia alionya.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya na mkoa huo kusimamia suala hilo na kuhakikisha linatokomezwa kabisa, ili kukabiliana na mimba za utotoni na mabinti waelekeze nguvu kwenye mambo ya msingi kama elimu.

Mkuu wa Nchi alisema serikali inawajengea mazingira rafiki ya kilimo ikiwamo kuwapa pembejeo za kilimo ili kuwasaidia kuboresha mavuno yao na kujiinua kiuchumi, hivyo waache kutumia fedha hizo kwa mambo ambayo hayana manufaa kwao na taifa.

**VIONGOZI WAJIPIME**

Rais Samia pia alioneshwa kushangazwa na kitendo cha kukosekana Sh. milioni 300 kwa ajili ya kujenga jengo la kuweka mashine ya mionzi (X-ray) iliyonunuliwa na serikali kwa fedha kwa lengo la kuboresha huduma za afya huku akiwataka viongozi kujitafakari.

"Tulisema asilimia 40 ya mapato ya kila halmashauri ielekezwe kwenye shughuli za maendeleo. Sasa ni shughuli zipi za maendeleo? Serikali inaleta mashine ya kuhudumia watu, mashine ipo stoo inasubiri serikali ilete fedha ya kujenga jengo la mashine, halmashauri hampo makini, watendaji wa halmashauri jitizameni tena," Rais alionya.

Vilevile, alikemea viongozi wanaotumia nafasi zao vibaya kuwanyonya wakulima kwa kufungua mifuko ya maendeleo na kuwakata wakulima Sh. 20 kwa kila kilo ya mazao kwa ajili ya mifuko hiyo wakati haipo kisheria na haikaguliwi.

Akizungumzia kero ya maji, Rais Samia alisema serikali imejipanga kutumia vyanzo mbalimbali vya maji vinavyopatikana mkoani humo ikiwamo Mto Ruvuma kuondoa changamoto hiyo.

Vilevile, alisema serikali imeanza safari ya kuondoa adha ya umeme mkoani humo na kuwataka wananchi wawe na subira wakati suala hilo linafanyiwa kazi na matunda watayaona.

"Kwa sasa mkandarasi yupo kazini kuunganisha Masasi kwenye Gridi ya Taifa kutokea Ruvuma. Lakini kuna mkandarasi ambaye anatoa umeme Ruangwa kupitia Nangugwa na utakuwa tayari ifikapo Desemba mwaka huu," alisema.

**KOROSHO**

Rais Samia pia alisema ili kuongeza bei ya korosho, serikali ina mpango wa kujenga kongani ya viwanda cha kukoboa zao hilo Wilaya ya Nanyumbu, ili kuongeza thamani na maganda yake kukamuliwa mafuta na kuuzwa.

"Lakini niungane na Waziri (Hussein Bashe) kutoa wito kwa wana Masasi, tunaona uvivu kusafisha mikorosho na badala yake tunachoma moto. Unapochoma moto kwanza unaunguza mikorosho na unaifanya isitoe matunda ya kutosha, la pili unaharibu mazingira," alisema.

Rais alisema serikali imejitoa kukuza kilimo kwa kiasi kikubwa na kuwataka wananchi kuunga mkono juhudi hizo kwa kuongeza bidii katika uzalishaji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengewa, alisema katika bajeti ya mwaka 2023/24, mkoa huo umetengewa Sh. bilioni 6.1 kwa ajili ya kujenga shule moja ya sekondari katika kila halmashauri.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, alisema wizara imefanyia kazi mgogoro wa Gereza la Namajani. Sasa wananchi watarudishiwa maeneo kwa ajili ya shughuli zao.

Alisema utatuzi wa mgogoro wa Kijiji cha Ngalole umefikia asilimia 95 huku akiahidi maboresho katika tume ya mipango ya matumizi ya ardhi ili iendane na kasi ya serikali.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema kuwa baada ya Wizara ya Ardhi kupanga maeneo yatakayotumika kwa ajili ya wafugaji, atahakikisha anajenga miundombinu ya unyweshaji mifugo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliwaeleza wakulima wa Wilaya ya Masasi kuwa hawatolipia ruzuku za zao la korosho kwa msimu huu na ujao.

Aliwasisitiza kwenda kujiandikisha katika Bodi ya Korosho kwa ajili ya kupata pembejeo za kilimo kwa kuwa zinatolewa kulingana na idadi ya mikorosho na kuwa serikali inafanyia kazi changamoto ya kupewa pembejeo pungufu ikiwamo mbolea.

Vilevile, aliwataka wakulima kulima kipindi cha masika kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame, hivyo majani kuwa ya njano, huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kuwapatia pembejeo.

# Watatu wanaosadikiwa majambazi wauawa Kenya

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU watatu akiwamo Mtanzania, Ibrahim Chacha, maarufu mchungaji, wanadaiwa kuuawa na polisi nchini Kenya wakituhumiwa kuwa majambazi.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi katika eneo la mji wa Isebania, Kenya na Sirari, Tanzania, Mwenyekiti wa Haki za Binadamu Kurya West, Peter Masaithe, alisema matukio ya uhalifu yameshamiri kwenye vijiji hivyo.

"Ninasikitishwa sana na vitendo vya uhalifu vilivyoshamiri kwenye mipaka yetu, watu wanafanya matukio sehemu mbalimbali wanakuja kujificha miji ya mipakani kwa ajili ya kufanya uhalifu halafu wanatoroka kwenda upande mwingine," alisema.

Alisema jana alipokea taarifa kuwa watu watatu wanaosadikiwa ni majambazi waliuawa na polisi katika eneo la Kisii na baada ya upekuzi walikutwa na silaha.

"Tunawaomba wananchi wa pande zote Kenya na Tanzania kushirikiana kukabili uhalifu ambao ni tishio kwa usalama wa watu na mali zao," alisema Peter.

Kamanda wa Polisi Kaunta ya Kisii, Charles Kasesa, alikaririwa na vyombo vya habari nchini Kenya akithibitisha kuuawa kwa watu hao.

"Majambazi hao walifanya unyang'anyi wa kutumia silaha maeneo mbalimbali, Septemba 4, mwaka huu, walivamia na kujeruhi watu kisha wakapora fedha katika 'super market' hapa Kisii, walitoroka kwa pikipiki."

Aidha, alisema tangu wakati huo walikuwa wanawasaka waliohusika hadi Septemba 14, mwaka huu, walipofanya uhalifu katika eneo la Soneka ambalo polisi walikuwa wameweka mtego uliowanasa na kuwaua kisha kwenye upekuzi waliwakuta na bunduki aina ya AK 47.

Kamanda Kasesa aliwataja waliouawa ni Wansato Ngocho, mkazi wa Kijiji cha Nyamaranya Isebania, Joseph Daniel, mkazi wa Gukihuru Masangura wote raia wa Kenya na Mtanzania Ibrahim, mkazi wa Sirari.

Alisema miili ya watu hao imehifadhiwa Hospitali ya Kisii huku Kamanda huyo akiwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa polisi ili kukabiliana na uhalifu huo.

Diwani wa Kata ya Sirari, Amos Sagara na Mwenyekiti wa Kijiji cha Kanisani, Tanzania, Nyamagige Gesamarwa, walisema ni muhimu wananchi wakawafichua wahalifu ili hatua madhubuti zichukuliwe.

Alisema ni muhimu wananchi wakatoa taarifa wanapoona kuna wageni kwenye vitongoji na vijiji vyao ili kutambua wanaoishi nchini bila kibali.

Kadhalika alisema siku zote walikuwa wanafahamu kuwa Ibrahimu ni mchungaji ambaye alionekana akitumia usafiri wa bodaboda kuhubiri kumbe alikuwa na shughuli nyingine ambazo ni kinyume cha sheria.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kanisani, alikokuwa anaishi Ibrahim alisema alihamia eneo hilo miaka miwili iliyopita akitokea Mugumu, Serengeti akihubiri injili kiasi cha kufahamika ni mchungaji wa Kanisa la Umoja Foundation.




Ofisa Mkuu wa Uendeshaji CPS, Katrin Dietzold, akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari mjini Fumba Town, Zanzibar mwishoni wa wiki katika mahafali ya kuwapongeza wanafunzi waliohitimu programu ya CPS STEM, mpango unaowezesha wahitimu wa kike waliosoma masomo ya sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Laban aifagilia Ruvuma kuwapo fursa nyingi kilimo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amelitaja eneo lenye fursa nyingi za uwekezaji Ruvuma kuwa ni sekta ya kilimo.

Akizungumza wakati anafungua kongamano la Biashara na Uwekezaji la Mkoa, Kanali Thomas aliyataja mazao makuu ya biashara yanayozalishwa kuwa ni kahawa, korosho na tumbaku.

Mazao ya chakula na biashara ameyataja kuwa ni mahindi, ufuta, soya, mbaazi, alizeti, mpunga, maharage, tangawizi na mazao mengine ya bustani.

"Mkoa wa Ruvuma ndiyo mzalishaji mkubwa wa kwanza wa mazao ya nafaka nchini, hata hivyo lengo la mkoa ni kuzalisha zaidi hivyo tunahitaji uwekezaji kwenye viwanda vya mbolea na viuatilifu kwenye kilimo," alisema RC Thomas.

Alisema Mkoa wa Ruvuma umetenga maeneo ya uwekezaji katika kilimo cha pamoja yenye jumla ya hekta 25,017 ambazo zimetambuliwa na zinatakiwa kuwekezwa.

Alisisitiza kuwa Mkoa wa Ruvuma una mazao ya kutosha kuanzisha viwanda vya uchakataji na kwa mwaka 2022/2023 ulizalisha tani 25,284.5 za korosho, 13,700 kahawa, 7,970.2 ufuta, 5,152.3 soya, 2,846.9 mbaazi na 731,224 mahindi.

Alisema katika msimu wa mwaka 2022/2023 Mkoa wa Ruvuma umezalishaji tani 1,598,163 za mazao ya chakula na kuufanya kuwa na ziada ya tani 1,043,525.

Kadhalika, alisema mkoa huo una mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuna jumla ya hekta 197,108.2 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hadi sasa ni hekta 7,388.3 pekee zilizoendelezwa sawa na asilimia 3.7.



RIPOTI YA UCHUNGUZI -3

# Vikundi hewa vilivyoishtua serikali ulaji mabilioni

Na Mwandishi Wetu

**KATIKA sehemu ya pili ya ripoti hii, kulikuwa na ufafanuzi wa mbinu zinazotumiwa na baadhi ya watu kujipatia mamilioni ya shilingi kupitia mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum, pia upendeleo kutokana na vyama vya siasa wanakotoka wanufaika wa mikopo hiyo na baadhi ya watendaji wa serikali na viongozi wa kisiasa kuwa sehemu ya udanganyifu. Sasa endelea...**

---

### SAMIA ASHTUKA

MNAMO Machi 29 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22, aliagiza kuangaliwa upya taratibu za utoaji mikopo hiyo.

CAG Charles Kichere amebainisha katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22 kuwa Sh. bilioni 88 zilizotolewa na halmashauri kama mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu hazikurejeshwa, shida kuu ikiwa utaratibu mbovu wa utoaji mikopo hiyo na ufuatiliaji hafifu.

"Sh. bilioni 88 zimekwenda, hazijakusanywa na hazikusanyiki, na hii ni kwa sababu vikundi vinavyopewa ni hewa, uadilifu kwa madiwani ni hewa na pili wanaopewa wanaona wamepewa na madiwani wao, hawaoni umuhimu wa kurejesha. Kwahiyo, tunahitaji marekebisho makubwa," aliagiza Rais Samia.

Marekebisho yanayotajwa na Rais Samia yanahusu kubadili mfumo wa utoaji mikopo hiyo kutoka halmashauri ili kazi hiyo ifanywe na benki ambayo itakuwa imeteuliwa na serikali kusimamia jambo hilo, ushauri ambao ulitolewa na CAG katika ripoti ya mwaka 2020/21.

"Njia itayotufaa ni ya kutumia mfumo wa benki, tupige hesabu ya asilimia 10 inayohitajika katika halmashauri husika kisha ikakae benki, wanaohitaji mikopo watakwenda benki, kwa sababu benki uwe unataka au hutaki, lazima utarejesha," Rais aliagiza.

### JICHO LA CAG

Kwa mujibu wa CAG, katika miaka mitano sita ya fedha iliyopita (2016/17-2021/22), jumla ya Sh. bilioni 192 hazijarejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, CAG Kichere alibaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo hiyo.

CAG Charles Kichere alibainisha kuwa kwa mwaka huo wa ukaguzi, halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo. Kwa mujibu wa CAG, hali iliyobainika katika ukaguzi wake wa mwaka 2020/21 ni mwendelezo wa kile alichokibaini katika miaka mitano iliyopita kuhusu mikopo hiyo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa.

| Mwaka | Hal. | Kisichorejeshwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 155 | Bilioni 47/- | 70 |
| 2019/20 | 130 | Bilioni 27.79/- | 65 |
| 2018/19 | 111 | Bilioni 13.79/- | 59 |
| 2017/18 | 90 | Bilioni 10.04/- | 59 |
| 2016/17 | 84 | Bilioni 5.81/- | 63 |

**Jedwali la mikopo isiyorejeshwa inayotolewa na serikali kwa makundi maalum kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri nchini. CHANZO: RIPOTI YA CAG 2020/21.**

Ripoti ya CAG kwa mwaka 2019/20, inaonesha Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam ilitoa mikopo ya Sh. milioni 698.7 kwa vikundi hewa 34, wakati Manispaa ya Temeke ilitoa Sh. milioni 178.536 kwa vikundi vya aina hiyo tisa.

CAG pia alibaini Manispaa ya Temeke ilitoa mikopo ya Sh. milioni 147.26 kwa vikundi vitano vilivyokuwa na wanachama wenye ajira rasmi kinyume cha utaratibu.

Katika ripoti hiyo, Halmashauri ya Meru iliyoko mkoani Arusha imetajwa kutoa mikopo ya Sh. 18,700,000 kwa vikundi hewa huku Halmashauri ya Mji wa Geita ikiongoza kwa kuwa na vikundi 396 vilivyokopa na vimeacha biashara/miradi huku vinadaiwa Sh. bilioni 1.05.

CAG pia anabainisha halmashauri nyingine zilizokaguliwa na kukuta vikundi hewa na kiasi cha fedha kilichotolewa katika mabano ni Maswa (Sh. milioni 179.66), Geita (Sh. milioni 176.52), Jiji la Arusha (Sh. milioni 141.32), Tandahimba (Sh. milioni 121.54), Busega (Sh. milioni 32.92), Monduli (Sh. milioni 105.38) na Mbulu Mji (Sh. milioni 27.77).

Katika uchunguzi wake, mwandishi alibaini vikundi hivyo viliundwa mahsusi kwa ajili ya kukopa na baada ya kuchukua mikopo, vilifunga biashara.

Mwandishi pia alibaini kuwapo ikundi hewa ambavyo vinaundwa wakati wa utaratibu wa kupata fedha hizo na wanapozipata vinavunjwa baada ya kila aliyehusika kupata mgawo wake.

Baadhi ya vikundi hivyo vinaundwa na watumishi wa serikali na viongozi wa kisiasa, hivyo kuwanyima fursa ya kukopa wananchi wanaostahili kupata mikopo hiyo.

Ni kadhia inayokinzana na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016-2021), ambao pamoja na mambo mengine, unakusudia kuweka mazingira wezeshi kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kujiajiri na kushiriki katika shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Mikakati ya kutimiza lengo hilo iliyoainishwa katika mpango huo ni utoaji wa mikopo yenye gharama na masharti nafuu kwa makundi hayo.

Vilevile, vitendo hivyo vinakwaza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025, yenye dhima kuu ya kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

### RIPOTI YA 2021/22

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22, CAG Kichere anabainisha kuwa Sh. bilioni 88 zilizokopeshwa na halmashauri kwa makundi maalum kwa mwaka huo wa fedha, hazijakusanywa.

CAG anabainisha kuwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunatokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo, akifafanua kuwa mamlaka za serikali za mitaa husika zilitoa mikopo kabla ya kufanya uchambuzi wa kina wa historia ya ulipaji wa kikundi na kupitia mapendekezo ya mradi husika ili kuhakikisha kikundi kina uwezo wa kurejesha mkopo kwa wakati.

Vilevile, CAG anasema amebaini hakuna ufuatiliaji wa karibu wa kukusanya marejesho ya mikopo ambayo haijalipwa kutoka kwenye vikundi.

Anasema ni dhahiri kuwa kutorejeshwa mikopo kunaweza kuathiri mfuko, hivyo kuufanya usiwe endelevu.

Ili kufikia lengo na uendelevu wa mfuko, CAG anasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo hayajalipwa.

Pia anaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

CAG anataja dosari nyingine katika mikopo hiyo ni kutoshirikishwa kwa wataalamu wa usimamizi wa mikopo katika mchakato wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

Anafafanua kuwa Kanuni ya 8 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019, inataka taratibu zote za wa mikopo zisimamiwe na mamlaka za serikali za mitaa.

"Nilibaini kuwa uhakiki wa vikundi vilivyoomba mikopo ulikuwa haufanyiki kabisa kabla ya mikopo kutolewa. Hii ni kutokana na ukosefu wa utaalamu wa kufanya uhakiki unaostahili katika mikopo.

"Pia kukosekana kwa usaidizi wa kisheria kutoka katika vitengo vya sheria kuhusu masuala ya bima hasa kwa mikopo inayotolewa kwa vijana, ambao mara nyingi walikuwa wakinunua pikipiki na bajaji. Mfuko hauna sera ya jinsi ya kushughulikia mikopo isiyolipika (NPL)," anasema.

CAG Kichere anabainisha kuwa kati ya madeni hayo, yapo ambayo yameonekana dhahiri hayatalipika kutokana na kuwa chechefu au madeni hewa na hivyo kuendelea kuudhoofisha mfuko.

Katika hilo, CAG anasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo hayajalipwa.

"Zaidi ya hayo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inashauriwa kuandaa sera ya mikopo isiyolipika (NPL) ili kusimamia mikopo inayotolewa kwa vikundi husika," CAG anawasilisha hoja yake.

Kinachoshuhudiwa sasa katika usimamizi wa mikopo hiyo, ni mwendelezo wa hujuma zilizotokea wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Rais Jakaya Kikwete, pale serikali yake ilipokuja na mikopo ya Sh. bilioni moja kila mkoa kwa ajili ya wajasiriamali, maarufu Mabilioni ya JK.

Ni fedha zilizotumiwa vibaya kiasi cha baadhi ya watendaji kukamatwa kwa wizi wa fedha hizo, huku lengo la kusaidia wajasiariamali likiishia njiani.

### KUHUSU MIKOPO HII

Inaporejewa historia ya mikopo ya halmshauri kwa makundi maalum, mwaka 1993 serikali kupitia Bunge, ilianzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambapo wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana.

Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana.

Mnamo mwaka 2019, serikali kupitia Bunge, ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kifungu cha 37A(1) cha Sheria hiyo kinazitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa.

Vilevile, Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5/04/2019) zinataka mamlaka zote za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Madhumuni ya mfuko huo ni kuongeza uwezeshaji kiuchumi kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kufanya shughuli za kiuchumi ili kuboresha kiwango chao cha maisha.

Ili kuwezesha mfuko uwe hai, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa fedha zinazokopeshwa kwa vikundi zinarejeshwa kwa mujibu wa makubaliano kati ya mamlaka za serikali za mitaa na vikundi vinavyonufaika na mkopo huo.



Wananchi wa Mangaka wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara wakiwa katika mkutano wa hadhara kumsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan jana. **PICHA: IKULU**

# Wananchi wapendekeza kuondolewa polisi jamii

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Kibaha wamependekeza kuondolewa kwa polisi jamii kwenye kata kwa madai kwamba sasa wanatuhumiwa na vituo vya polisi kukamata wahalifu, jambo ambalo si lengo la uanzishwaji wake.

Vilevile, wameomba kazi ya kunyonga wanaohusika na mauaji iundiwe kitengo chake badala ya kuacha jukumu hilo kwa Rais kwa kuwa kuna ongezeko la watu wanaofanya vitendo vinavyosababisha wahukumiwe kunyongwa.

Wakitoa maoni yao mwishoni mwa wiki mbele ya Tume ya Haki Jinai, wananchi hao akiwamo Hawa John, alisema polisi jamii hao kutoka kwenye kata wamekuwa wakikaa polisi na kutumwa kukamata watuhumiwa.

"Hawa polisi jamii wako sana kwenye kata, unapofika kuelezea tukio lako polisi unaambiwa uwape fedha, ili wakamkamate mtuhumiwa. Hili jambo kwetu ni kero, tunaomba tume ilifanyie kazi," alisisitiza Hawa.

Alisema baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi hawawalindi watu wanaotoa taarifa za wahalifu, akisema ni suala linalopaswa kuangaliwa ili kulinda usalama wao kwa kuwa wapo wanaopelekewa taarifa kuhusiana na wahalifu, lakini hao hao wanawataja watoa taarifa.

**HUKUMU YA KIFO**

Ramadhani Maulid alieleza katika mkutano huo kwamba, anatamani siku moja angeajiriwa na serikali ili akafanye kazi ya kunyonga watu waliohukumiwa kutumikia adhabu hiyo baada ya kukutwa na hatia ya kuhusika na mauaji.

Alisema zipo taarifa zinazoelezwa kwenye vyombo mbalimbali kuwa kwa miaka mingi adhabu hiyo imekuwa haitekelezwi nchini huku matukio ya mauaji yakiendelea.

Mwananchi huyo alisema ni wakati sasa serikali kuliangalia suala hilo sambamba na kuajiri watu wenye roho ngumu kama yeye watakaotekeleza adhabu ya kunyonga.

"Unakuta mtu ameua kwa makusudi halafu anakwenda kukaa gerezani muda mrefu bila kunyongwa. Hilo haliwezekani.

"Kama mtu amekutwa na hatia ya kuua naye anyongwe, siyo unasikia wanaanza kusema haki za binadamu, kwani yeye alipokuwa anaua alikuwa hajui kuwa kuna haki za binadamu?" Alihoji?

Mjumbe wa tume hiyo, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema kutotiwa saini adhabu ya kifo kwa watu wanaohukumiwa kutumikia adhabu hiyo kwa muda mrefu sasa kumesababisha kuwapo mrundikano wa wafungwa na kwamba mapendekezo yao ni kuona suala hilo linaangaliwa upya.

Prof. Edward Hosea ambaye ni Mjumbe wa Tume ya Haki Jinai, alisema katika ufuatiliaji wao walibaini kwamba zipo sheria nyingi zinatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kulinda haki za wananchi ikiwamo utitiri wa majeshi uliopo ambao unapaswa kuangaliwa na kuundiwa sheria upya.

# Waziri Tax: Ushirikiano jeshi la Tanzania, China kuongeza tija

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, amesema ushirikiano mzuri wa Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Jamhuri ya Watu wa China unaongeza tija na ufanisi katika nchi hizo katika kubadilishana mbinu na uzoefu wa kupambana na ugaidi na uhaini wa baharini.

Dk. Tax alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akifunga mafunzo ya Muungano JWTZ Kamandi ya Wanamaji (Navy) na Kamandi ya Wanamaji ya China, yaliyolenga kubadilishana mbinu na maarifa ya kisasa ya kupambana na ugaidi katika bahari za nchi hizo.

"Tanzania na China tuna uhusiano mzuri na ni washirika wa masuala ya kijeshi. Leo ninafunga mafunzo haya, mkatumie vyema mbinu mlizobadilishana katika kupambana na ugaidi wa majini," alisema Dk. Tax.

Alisema ili kuimarisha JWTZ, waliandaa mafunzo hayo kwa askari na maofisa 151 kwa nchi zote mbili kwa ajili ya kuongeza ufanisi, kushirikiana, kupeana mbinu mpya na za kisasa katika kukabiliana na changamoto za ugaidi majini.

Alisema kuna haja nchi hizo ziendelee kushirikiana katika nyanja mbalimbali kwenye kukuza utendaji wa majeshi hayo na waliyojifunza bila kuhatarisha usalama wao wakati wote wa mafunzo.

"Mafunzo haya yalihusisha mazoezi makali, lakini yamekamilika bila majeruhi ni jambo la kuwapongeza na kuwataka wayatumie vyema wanaporejea kwenye vituo vyao vya kazi," alisema Dk. Tax.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Kituo cha Mafunzo Maalum Mapinga (CTC), mkoani Pwani.

# NIT yaweka mkakati uzalishaji wahandisi wanawake nchini

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimesema kitaendelea kuzalisha wahandisi wengi zaidi wenye weledi hususani wa kike ambao wana uwezo mkubwa wa kutoa huduma katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Mkakati huo unalenga kuunga mkono mipango ya serikali ya kuona Taifa linakuwa na rasilimali watu wa kutosha kwenye sekta ya usafiri na usafirishaji, hususani usafiri wa anga unaokua kwa kasi.

Katika Maadhimisho ya Siku ya Wahandisi mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Naibu Mkuu wa NIT anayeshugulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri, Dk. Prosper Mgaya, aliihakikishia serikali kuwa kupitia mikakati yao, katika miaka michache ijayo idadi ya wahandisi wanawake itaongezeka.

Kauli ya NIT imekuja baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuviagiza vyuo vikuu na vyuo vya kati nchini kuongeza uzalishaji wahandisi wanawake.

Waziri Mkuu alisema serikali kupitia Wizara ya Ujenzi itaweka miradi ya majaribio kwa wahandisi wanawake walioanzisha kampuni za ujenzi ili kuonesha umahiri wao.

Naibu Mkuu wa chuo alisema kuwa kupitia Mradi wa Benki ya Dunia wa Ujuzi wa Afrika Mashariki kwa Mabadiliko na Ushirikiano wa Kikanda (EASTRIP), NIT imeanzisha programu ya Ufadhili wa Ubora wa Usafirishaji (TES) ili kuweza kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike na kuzalisha wahandisi wengi zaidi katika eneo la sekta ya anga.

"Tumeanzisha ufadhili huu ili kusaidia wanafunzi wa kike wanaotaka kusoma programu za uhandisi wa ndege. Tunaelewa kuwa taifa lina uhaba wa wahandisi wa kike hasa katika sekta ya anga, hivyo tunaamini programu hii itaongeza idadi ya wahandisi wanawake katika matengenezo ya ndege," alisema.

Dk. Mgaya aliongeza: "Tumeweka vigezo ambavyo siyo tu ufaulu kwa msichana utamwezesha kupata nafasi, bali vigezo vya msingi vya kutoa ufadhili huu ni kuona wasichana kutoka familia maskini na hata familia za wakulima, wananufaika na ufadhili huu wa masomo.

"Katika kuhakikisha wanawake wengi wanasoma masomo ya sayansi, hivi karibuni tumetembelea shule za sekondari za mikoa ya Mtwara na Lindi ili kuhamasisha wanafunzi wa kike wa eneo hilo kusoma masomo ya sayansi.

"Kupitia ziara ya kutembelea shule za sekondari, timu ya NIT ilianzisha mpango wa ufadhili wa masomo kwa wanawake ambao hutolewa katika taasisi yetu kama hatua ya kuongeza udahili wa wasichana."

Baadhi ya wahandisi wa kike waliosoma NIT, walivitaka vyuo vikuu na vyuo vya kati nchini kutoa vipaumbele kwa wanawake wakati wa kudahili wanafunzi.

Subira Mwakyoma, mhandisi aliyesoma NIT ambaye sasa anafanya kazi katika Kampuni ya Ndege za Serikali (ATCL) kama mhandisi wa ndege, alisema: "Ninashauri NIT kuendelea kutoa vipaumbele kwa wanawake wakati wa kudahili wanafunzi katika kozi za uhandisi ambapo wanafunzi wa kike ni wachache kulinganishwa na wanaume.

"Kudahili wanafunzi wa kike wa kutosha katika uhandisi hasa kwenye sekta ya anga, kutatoa nafasi kwa wanafunzi wa kike na hivyo kuondoa dhana kwamba taaluma hii si ya kiume tu, bali ya wote."

Alibainisha kuwa kozi ya uhandisi wa usafiri wa anga aliyoipata NIT imemfanya ajiunge kwa urahisi ATCL kama mhandisi wa matengenezo ya ndege.

Mkufunzi Msaidizi wa Mafunzo wa NIT katika Uhandisi wa Usafiri, Gerwarda Mugh, alisema: "Tunawahimiza wasichana kusomea kozi za uhandisi katika taasisi yetu. Programu hizi si za wanaume tu kama wengi wanavyofikiri, bali wanawake wanaweza kufanya vyema zaidi."

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba, Yanga jipangeni kwa dakika 90 za pili mechi CAF

**MWISHONI** mwa wiki wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya klabu, Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga walianza vizuri katika mechi zao kwanza za raundi ya kwanza kuwania kutinga hatua ya makundi.

Simba ambayo ilikuwa ugenini nchini Zambia ililazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya wenyeji wao Power Dynamos, matokeo ambayo yanaiweka 50 kwa 50 kwani ili kutinga hatua ya makundi katika mchezo wa marudiano nyumbani Oktoba Mosi, mwaka huu, sasa inatakiwa kupata suluhu ama sare ya bao 1-1 au kushinda.

Lakini kwa upande Yanga, ambayo ikiwa ugenini nchi Rwanda, iliwachapa wenyeji wao Al-Merrikh ya Sudan kwa mabao 2-0, yenyewe inahitaji sare ama ushindi wowote au kutokubali kufungwa zaidi ya bao moja katika mechi ya marudiano Septemba 30, mwaka huu, ili kutinga hatua ya makundi.

Ikumbukwe Al-Merrikh inachezea mechi zake za nyumbani nchini Rwanda kutokana na hali ya machafuko ya kisiasa yanayoendelea kwao, Sudan.

Kwa ujumla wawakilishi hao wa nchi wamejiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, hususan Yanga inayotaka kutinga hatua ya makundi baada ya miaka 24, hata hivyo haitakiwi kubweteka kwa matokeo hayo kwani wapinzani wao nao wataingia 'msituni' kwa ajili ya kutaka kuja kupindua meza.

Kwenye soka hakuna linaloshindikana kwani siku zote kuna matokeo matatu, kushinda, kushindwa na sare, ambapo kila timu huweka malengo ya kwanza yakiwa kushinda, hivyo tunawakumbusha wawakilishi wetu hao wa nchini kuwa hizo ni sawa na dakika 45 za kipindi cha kwanza, wanapaswa kujipanga vema kwa zingine kama hizo za kipindi cha pili ili kujihakikishia nafasi hiyo.

Kikubwa katika maandalizi hayo ni kila mchezaji, na mabenchi yao ya ufundi kuwajenga kisaikolojia kwa kuwasisitiza kutobweteka na matokeo waliyoyapata ugenini kwa kutambua kwamba pia wapinzani wao wanaweza kuyapata hapa nchini.

Lakini licha ya matokeo hayo, Simba, Yanga zinapaswa kutambua kwamba kwa mechi za mfumo huo wa mtoano, huwezi kusema shughuli imeisha bali mpaka iishe kabisa kwa maana ya dakika 90 za pili.

Sisi tunaamini katika maandalizi, hivyo ni wakati sahihi kwa wawakilishi hao wa nchi kujiandaa kwa siku hizi takriban 12 kabla ya marudiano na kusahau matokeo yaliyopita na ifikapo siku ya mchezo kushuka uwanjani kama vile wamepoteza michezo yao ya kwanza.

Lakini pia kwa Singida Fountain Gate FC, ambayo jana ilishuka Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kuikaribisha Future FC ya Misri katika mchezo wao wa awali wa Kombe la Shirikisho Afrika, kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi, haina budi kusahau matokeoya jana na kujipanga kwa mechi ya marudiano ugenini.

Tunataka kuona wawakilishi hao wa nchi msimu huu wakiifanya Tanzania kuweka rekodi, kwanza kwa mara ya kwanza kuingiza timu mbili hatua ya makundi kwa msimu mmoja tangu kuanzishwa kwa michuano hiyo, lakini pia ikiwa na klabu tatu katika hatua hiyo kwenye michuano inayoandaliwa na CAF, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Hatuna shaka kabisa katika hilo, kwani kwa muda uliobaki na kwa sababu tayari wamewafahamu vema wapinzani wao, tunaamini wawakilishi hao wa nchi kwa ujumla watarudi katika uwanja wa mazoezi kufanya maandalizi ya kutosha na kwenda kupata ushindi wa kishindo kwenye mechi za marudiano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

## Simba, Yanga kuungana kimataifa huu ni mzaha

**TATIZO** kubwa kwa sasa tulilonalo baadhi ya Watanzania tunapenda sana maneno ya kisiasa, kupakana mafuta, mzaha na kutoambiana ukweli. Wakati mwingine hili ndilo linalotutafuna na kutopiga hatua ya kuelekea kunakohitajika.

Hivi majuzi nimesikia kauli za baadhi ya maofisa habari wa Klabu za Singida Fountain Gate, Yanga na Azam kuwa timu hizo zimeungana kwa ajili ya kuhakikisha timu za Tanzania zinapata ushindi.

Ali Kamwe kabla ya kwenda nchini Rwanda, Thabit Zacharia na Hussein Massanza walikuwa wakizunguka studio mbalimbali kuhamasisha mashabiki kwenda uwanjani kuishangilia Singida katika mechi yao ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Future kutoka nchini Misri iliyochezwa jana Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Katika safari hiyo ya kuzungukia vyombo vya habari hakuwapo Ofisa Habari wa Simba, Ahmed Ally na alipoulizwa alisema alikuwa na kazi zingine hasa maandalizi ya safari ya kwenda Zambia, lakini yupo pamoja na hilo.

Hili la maofisa habari wa klabu kubwa za Simba na Yanga kuungana kupigia debe mechi za Taifa Stars, Azam, Singida United, hata Biashara United na Namungo ikiwezekana wanaweza kuungana na kufanya kazi pamoja kuita watu na kupeana mbinu za hapa na pale kama wenyewe wanavyosema.

Hata hivyo, sidhani kama wanaweza kuungana kwa ajili ya kusapoti mechi zao wenyewe.

Katika umri wangu huu sijawahi kuona kitu kama hicho na hata kama kikitengenezwa, mwisho wa siku kitaharibika tu kama ilivyokuwa mwaka 1993 wakati mashabiki wa Yanga walipoanza kuimba. "uzalendo umetushinda" pale Stella Abdijan ilipofunga bao la pili dhidi ya Simba katika mechi ya fainali Kombe la CAF.

Kupeana mbinu kwa timu hizi mbili ndiyo kabisa haiwezekani na haitowezekana kwa sababu siku zote hizi timu zinachekeana jino pembe. Hakuna mashabiki wanaotaka timu nyingine ifanikiwe kwa sababu hata kama watafanya hivyo, wa kwanza kupata machungu ya kubezwa watakuwa wao.

Simba na Yanga wanatakiana mema mdomoni tu, lakini mioyoni hakuna anayetaka mmoja afanikiwe. Ukitaka kujua hilo, fikiria kama timu moja itaondolewa kwenye michuano ya kimataifa, kwa sababu zimeungana kwa ajili ya mechi za kimataifa, mmoja anaweza kwenda kumsaidia mwenzake kuhamasisha watu kwenda uwanjani?

Eti umuone Ahmed akiwahamasisha Wanayanga wakaitazame mechi Yanga ikicheza dhidi ya Al-Merrikh, au Kamwe akiwaambia Wanasimba wasikose uwanjani kuona timu yao ikicheza dhidi ya Power Dynamos. Ni mzaha mtupu huu, tuaache tu waipambanie Timu ya Taifa, Taifa Stars tu.

Mimi nadhani hizi timu ziachwe kila mmoja ajipambanie mwenyewe, ila tu kusiwe na kufanyiana hujuma na kuwasaidia wapinzani wanapokuja nchini kama ilivyokuwa huko nyuma.

Hilo peke yake linatosha sana. Serikali na Shirikisho la Soka wawe wakali na makini kwa watu wanaokwenda kuwapokea wageni Uwanja wa Ndege, kuwapa mbinu wapinzani, viongozi kuvaa jezi za timu pinzani au kuonekana kuwa karibu nao.

Hapa ndipo wanapotakiwa kuchukua hatua kwa manufaa ya nchi, lakini siyo kwa maofisa habari wa timu hizo kuungana au klabu hizo kupeana mbinu, hili haliwezekani kufanyika.

Kitu pekee ambacho hakina athari ambacho inabidi kiachwe ni mashabiki kwenda kushangilia wapinzani. Hii ni haki yao hawezi kumpangia mtu cha kushangilia, lakini si kuhujumiana.

Simba na Yanga ni timu kubwa na kila mmoja anajua mbinu za kushinda mechi zake bila msaada wa mwenzake. Hizi timu ni watani wa jadi na wapinzani, waachwe waendelee kuwa hivyo, ila kimataifa mamlaka ilindwe kwa wanaotaka kufanya hujuma, lakini kusaidiana inaonekana ni siasa tu.

## HABARI KITAIFA

# Biteko awaonya watumishi EWURA kuvujisha taarifa kupaa bei mafuta

**Na Christina Mwakangale**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amewaonya baadhi ya watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), wanaovujisha siri za mamlaka hiyo.

Watumishi hao wanadaiwa kuvujisha siri hizo ili kuwalinda wafanyabiashara na kusababisha uhaba wa mafuta siku chache kabla ya kutangazwa bei mpya ya kila mwezi.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Biteko ameiagiza Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi Mkuu EWURA, kuchunguza watumishi hao na kujiridhisha kama wako waaminifu ili wapewe somo namna ya kuwa waaminifu.

Biteko alisema hayo mwishoni mwa wiki alipozuru na kuzungumza na menejimenti, watumishi wa mamlaka hiyo kwenye ofisi za EWURA mkoani Dar es Salaam.

"Zipo taarifa tunazipitia za watu wachache humu ndani (EWURA) ambao si waaminifu wanajihusisha na vitendo vidogo vidogo vya hapa na pale. Tunataka kufanya operesheni kwa wahusika lakini utakuta wote wanaotakiwa kufanyiwa operesheni wanapata taarifa siku hiyo hiyo.

"Siku ya ukaguzi utakuta wote wana dharura. Kuna 'crisis' (uhaba) ya mafuta inatokea, tunaenda kukagua unakuta watu wote wameshajua wamefunga na hawapo. Hii ni kwa sababu ndani ya EWURA wanazo taarifa wanazivujisha kwa watu. Tumeamua kufanya mageuzi makubwa ya kupitia rasilimali watu tuliyo nayo ili tujiridhishe wale waaminifu tuendelee kufanya nao kazi na wasio waaminifu tuwafundishe kuwa waaminifu," alisema.

Kuhusu hali ya mafuta nchini, Dk. Biteko alisema uhaba unaotokana na wazalishaji wa nishati hiyo ikiwamo pesa za kigeni, hivyo mikakati inaandaliwa ili nchi kuja na mipango ya muda mrefu ambayo itakuwa endelevu.

"Changamoto ya mafuta si Tanzania pekee bali duniani kwa ujumla. Pamoja na changamoto na sababu ambazo ziko nje ya Tanzania, bei, ukosefu wa dola, ziko za ndani ambazo ni lazima tuziangaliwe ili kupunguza mzigo kwa wananchi. Kazi ya EWURA ni kupitia na kufanya utafiti, kujiridhisha kwamba bei ni halisi?" Alibainisha Dk. Biteko.

Alisema kupitia EWURA, Wizara na Wakala wa Uagizaji Mafuta Pamoja (PBPA), wahakikishe uhalisia uliopo kwenye bei na si vinginevyo, ili kuleta ahueni kwa watumiaji wa nishati hiyo muhimu nchini.

"Sisemi kwamba tunataka kushusha bei, tujiridhishe, kama bei mafuta kuleta nchini tumeambiwa ni dola 200. Je, kweli ni dola 200? Na kama si hiyo kwa nini ilipandishwa? Jambo ambalo linawapa simanzi Watanzania ni kila mara bei inapotaka kubadilika kipindi hicho hicho, utaona mafuta yanaadimika. Baada ya muda bei ikitoka, unaona hali inarudi kama kawaida, huu ndio mchezo ambao Watanzania hawawezi kufanyiwa kwa muda wote.

"Lazima wafanyabiashara tujue pamoja na leseni ya biashara unayopewa pamoja na lengo lako ndio ni faida, kukuza mtaji, lakini wanahudumia Watanzania, ili biashara yake isitatizike. Kama mtu alikuwa na kiwanda chake akafunga na alifanya biashara ya daladala, ili anunue gari lingine, akaacha, hata wewe utaathirika. Wafanye biashara kwa uaminifu," alisema.

Alisema kwamba serikali inaendelea kukabiliana na changamoto ya nishati hiyo nchini, hivyo fursa ya magari yanayotumia nishati ya gesi nchini ikuzwe, ikiwamo serikali kuanzisha mfumo wa matumizi wa magari ya yanayotumia gesi asilia.

"Wazalishaji wakubwa wamepunguza mahitaji lakini mahitaji yameongezeka kwa sababu shughuli za uchumi zimeongezeka. Watu wanajenga viwanda, wananunua magari, lazima tufikiri kimkakati ili kuziba hilo pengo. Mpango wa serikali ni wa magari yanayotumia gesi asilia. Sasa kwa nini hatuongezi hiyo kasi, vituo vijengwe zaidi, tuanze serikali," alisema.



Mtaalamu wa Macho kutoka Hospitali ya KSIJ jijini Dar es Salaam, Ain Sheriff (kushoto), akizungumza jana katika mkutano na waandishi wa habari wakati akitoa tathmini ya kambi ya matibabu iliyofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Wakili Kibatala adai polisi kutoka Zanzibar amejifanya dada wa kazi

**Na Grace Gurisha**

WAKILI wa Utetezi, Peter Kibatala katika kesi ya mauaji ya dada wa marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Aneth Msuya, amedai mahakamani wana taarifa aliyekuja kutoa ushahidi kama dada wa kazi wa marehemu si Getruda Mfuru, bali ni askari kutoka Zanzibar.

Alidai hayo mwishoni mwa wiki mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akimwuliza maswali ya dodoso Mfuru ambaye ni shahidi wa 25 katika kesi ya mauaji namba 103 ya mwaka 2018 inayomkabili aliyekuwa mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela.

Wakili Kibatala alifikia hatua hiyo kutokana na majibu ya maswali ambayo alikuwa akimwuliza shahidi huyo kufuatia ushahidi aliotoa mahakamani kuhusiana na tukio la mauji ya Aneth, aliyeuawa kwa kukatwa shingo nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam.

**Kibatala:** Kama kweli wewe ni Getruda Mfuru ulianza kufanya kazi kwa Aneth kuanzia lini?

**Shahidi:** Januari 4, 2016 nilifika nyumbani kwake na kazi nilianza Januari 5, 2016.

**Kibatala:** Mtoto wa Aneth, Allan alikuwa analala wapi?

**Shahidi:** Alikuwa analala chumbani na mama yake.

**Kibatala:** Hiko chumba ni cha watoto au master bedroom?

**Shahidi:** Kilikuwa ni chumba cha dada Aneth.

**Kibatala:** Allan alikuwa anasoma shule gani?

**Shahidi:** Sikumbuki.

**Kibatala:** Sare zake za shule zilikuwa na rangi gani?

**Shahidi:** Siwezi kuzikumbuka.

**Kibatala:** Nani alikuwa anamwandaa kwenda shuleni?

**Shahidi:** Ni mimi.

**Kibatala:** Wewe ulikuwa unalala kwenye chumba gani?

**Shahidi:** Sikumbuki vizuri.

**Kibatala:** Ndiyo maana tuna taarifa kuwa wewe sio Getruda Mfuru. Tutajie majirani wa nyumbani kwenu, kwa upande wa mashariki, magharibi, kaskazini na kusini.

**Shahidi:** Kwa upande wa mashariki ni Ezekia Kundangila, Shikushaeli Ndosi, Wise na Kusini ni Puloteta Paul.

**Kibatala:** Ulisema ulisoma hadi kidato cha nne si ndio?

**Shahidi:** Ndiyo

**Kibatala:** Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi alikuwa anaitwa nani?

**Shahidi:** Mwalimu Kitomari.

**Kibatala:** Na sekondari je?

**Shahidi:** Sikumbuki.

**Shahidi:** Yaani hukumbuki halafu ulisema ulisoma hadi kidato cha nne.

**Shahidi:** Ndiyo.

**Kibatala:** Birthday ya baba yako ni lini?

**Shahidi:** Siwezi kukumbuka birthday ya Baba yangu.

**Kibatala:** Wewe ni Ofisa wa Polisi Kituo chako cha kazi ni polisi Zanzibar.

**Shahidi:** Mimi sio ofisa wa polisi na sijawahi kuwa polisi.

**Kibatala:** Aneth alikuwa anatuhumia gari aina gani?

**Shahidi:** BMW X 5 rangi ya silver.

**Kibatala:** Umekumbuka kuja na kitambulisho chako cha NIDA.

**Shahidi:** Nilishasema kitambulisho changu nimekiacha nyumbani Moshi.

**Kibatala:** Ile 20,000/- aliyokupa ilikuwaje?

**Shahidi:** Alinitishia kwanza ndipo akanipa 20,000/-.

**Kibatala:** 20,000/- ni sehemu ya kitisho?

**Shahidi:** Nimeshasema alinitishia kwanza ndipo akanipa.

**Kibatala:** Ile 20,000/- ulifanyia nini?

**Shahidi:** Sikumbuki nilifanyia nini wala sikumbuki niliiweka wapi.

**Kibatala:** Huyo rafiki yako Sabri ni kweli alikushauri uende polisi?

**Shahidi:** Ni kweli, Sabri alinishauri kwenda kuripoti polisi, kutokana na vitisho mimi sikwenda.

**Kibatala:** Mama wa watoto watatu bado ukaona usiende kuripoti polisi?

**Shahidi:** Kimya.

**Kibatala:** Ulipofika nyumbani kwenu Moshi, Masama, nani ulimwambia kuhusu tukio hilo?

**Shahidi:** Mama yangu mzazi.

**Kibatala:** Na yeye alichukua hatua gani?

**Shahidi:** Mama yangu alikuwa mgonjwa, hakuweza kuchukua hatua yoyote.

**Kibatala:** Unasali kanisa gani?

**Shahidi:** KKKT Masama, Moshi.

**Kibatala:** Mchungaji wako anaitwa nani?

**Shahidi:** Elihusu Kimaro.

**Kibatala:** Ulimwambia Mchungaji Kimaro mambo mazito haya?

**Shahidi:** Sikumwambia na pia sikuwa na mawazo ya kumwambia mchungaji.

Katika kesi hiyo, Mrita ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016, anadaiwa amekiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Kampuni nchini zapata neema Afrika Magharibi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

UNUNUZI wa ndege ya mizigo uliofanywa na serikali umeanza kuleta matunda baada ya kampuni kufikisha kwa wakati bidhaa zinazozalishwa nchini kwenye masoko ya nchi za Afrika Magharibi ikiwamo Algeria, Nigeria, Morocco na Ghana.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa bei ya bidhaa muhimu na vyakula nchini kwa kipindi cha Septemba, mwaka huu. Dk. Kijaji, alisema kabla ya ununuzi wa ndege hiyo, wafanyabiashara hao walikuwa wakilazimika kusafirisha bidhaa zao kupitia nchi za Ulaya na Bara la Asia ili kuyafikia masoko ya nchi hizo.

"Tunampongeza sana Rais Dk. Samia Hassan Suluhu, alipotununulia ndege ya mizigo inayoendeshwa na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), imeturahisishia kuyafikia masoko ya Afrika Magharibi," alisema.

Alisema baada ya serikali kufungua fursa za masoko kwenye eneo huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), kampuni nne zinapeleka bidhaa nchi za Algeria (kahawa), Nigeria na Ghana (katani) wakati Morocco (viungo vya vyakula) kwa kutumia ndege hiyo.

Alisisitiza kuwa serikali imeendelea kufungua mipaka ili kupata fursa katika nchi rafiki ambazo wamekubaliana nazo kibiashara, ikiwamo India iliyonunua mbaazi kwa kiwango kikubwa, Japan, Marekani na China ambazo zimefungua soko la bidhaa za nchini kwa asilimia 98.

Akizungumzia mwenendo wa bei ya vyakula nchini, alisema mahindi kwa mwezi huu ni kati ya Sh. 750 na Sh. 1,500 kwa kilo.

Alisema bei hiyo imeonyesha uhimilivu ikilinganishwa ilivyokuwa bei ya juu ya mwezi uliopita ambayo kilo ilikuwa ikiuzwa kwa Sh. 1,500.

Kijaji alisema bei ya chini ya mahindi imepungua kwa asilimia 11.8 sawa na kupungua kwa Sh. 100 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya chini ya Agosti ambayo ilikuwa ni Sh. 850 kwa kilo.

Kadhalika, alisema uchambuzi unaonyesha kwa wastani bei hiyo imepungua kwa asilimia 1.7 kwa mwezi huu.

Kuhusu bei ya mchele kwa mwezi huu, alisema ni kati ya Sh. 1,900 na Sh. 3,500 kwa kilo na imepanda kwa asilimia 2.9 sawa na ongezeko la Sh. 100 kwa kilo ikilinganishwa na mwezi uliopita ambayo ilikuwa ni Sh. 3,400 kwa kilo.

Kijaji alisema sukari kwa Septemba ni kati ya Sh. 2,800 na Sh. 3,200 kwa kilo, bei ya juu na chini kwa mwezi huo zimeonyesha uhimilivu kwa kutobadilika ikilinganishwa na Agosti ambao zilikuwa ni Sh. 2,800 na Sh. 3,200 kwa kilo.

Alisema mafuta ya kula ya alizeti kwa Septemba ni kati ya Sh. 4,000 na Sh. 8,000 kwa lita na bei ya juu ilongezeka kwa asilimia 6.7 sawa na ongezeka la Sh. 500 kwa lita ikilinganishwa na bei ya juu ya mafuta hayo Agosti ambayo ilikuwa Sh. 7,500 kwa lita.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema mkoa huo ni wenye fursa mbalimbali za mazao ya kilimo na wamejipanga kuongeza uzalishaji ili kufikia malengo ya kulisha taifa na ziada kuuza nje.




Meneja Mkuu wa NMB Foundation, Nelson Karumuna (kushoto), akizindua rasmi dirisha la pili la Ufadhili wa Masomo kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu 'NMB Nuru Yangu Scholarship' uliofanyika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam juzi. Katikati akishuhudia ni Mwenyekiti wa Bodi ya NMB Foundation inayofadhili wanafunzi hao, Ruth Zaipuna na kulia ni Mjumbe wa Bodi, Gladness Deogratias. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasimamizi viwanja vya ndege, bandari wapigwa msasa

**Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka wasimamizi wa sheria katika viwanja vya ndege na bandarini nchini kuendelea na usimamizi na udhibiti wa kemikali zinazodhibitiwa kwa kuzingatia ukomo wa matumizi yake.

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Mitawi, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua warsha kwa maofisa wa serikali waliopo katika Bandari ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali hizo chini ya Itifaki ya Montreal.

Mitawi alisema, maofisa forodha na wasimamizi wa sheria katika maeneo ya mipaka wana wajibu wa kusimamia uingizaji wa bidhaa mbalimbali nchini zikiwamo kemikali ambazo zimekuwa zikileta madhara katika jamii na kusababisha magonjwa ya saratani ya ngozi, upungufu wa kinga dhidi ya maradhi na kujikunja ngozi.

"Warsha hii ni muhimu kwenu na hii ni kutokana na majukumu yenu ya kila siku. Ninaamini mtajenga uelewa mkubwa zaidi katika masuala ya Tabaka la Ozoni na kuwa mabalozi wa kueneza elimu ya Ozoni kwa wengine ili sote kwa pamoja tuongeze juhudi za kuhifadhi," alisema Mitawi.

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kwa jamii, kuepuka matumizi ya vifaa na kemikali ambazo zinasababisha madhara kwa afya ya binadamu na mazingira ikiwamo athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema maofisa wa serikali na wasimamizi wa sheria mipakani ni wadau muhimu katika udhibiti wa uingizaji wa bidhaa hizo katika jamii, hivyo wana nafasi kubwa ya kuelimisha wananchi aina ya vifaa vinavyopaswa kutumika.

"Sote ni mashahidi kuhusu athari za kiafya kwa matumizi ya vifaa vyenye kemikali. Tumeshuhudia serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha za matibabu kwa wagonjwa wa saratani na pia, kumekuwapo na kiwango kikubwa cha joto siku hadi siku," alisema Mitawi.

Akifafanua, alisema nchi nyingi zinashuhudia athari za mabadiliko ya tabia ikiwamo ukame na ukosefu wa chakula katika maeneo mbalimbali duniani, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuchukua hatua kuhakikisha Watanzania wanabaki salama.

Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Kemilembe Mutasa, alisema kuelekea Siku ya Tabaka la Hifadhi ya Ozoni, Tanzania imeendelea kupata mafanikio makubwa katika udhibiti wa kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni.

"Tanzania siyo mzalishaji wa kemikali hizi, tumekuwa tukipokea kutoka nchi na nchi. Tumeandaa kanuni, sera, sheria na miongozo. Tumekuwa na mfululizo wa mafunzo haya kwa watendaji wa serikali ili kuwakumbusha wajibu wao katika maeneo yote ya udhibiti wa kemikali hizi," alisema Kemilembe.

# Serikali kuwezesha sekta ya bima kuimarika zaidi

**Na Grace Gurisha**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali itaendelea kutengeneza mazingira wezeshi kwa sekta ya bima nchini ili ikue zaidi na kuchangia uchumi wa taifa.

Katika hafla ya miaka 25 ya Kampuni ya Bima ya Alliance, alisema kampuni hiyo imefanya kazi kubwa kuhakikisha Watanzania wananufaika na bima kupitia bidhaa mbalimbali.

"Kampuni hii imeongeza bidhaa ya kukabiliana na hali ya hewa zisizotarajiwa kwenye sekta ya kilimo hivyo ni sekta muhimu," alisema Dk. Nchemba.

Alisema kwa kipindi hicho, kampuni hiyo imevuka mipaka hadi nchini Uganda.

Mwigulu alisema kwa kuwa serikali ya awamu ya sita moja ya maeneo ambayo imetilia mkazo katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na kama wizara wanaunga mkono kampuni hiyo kwa kuongeza bidhaa.

Pia kampuni hiyo itachangia Dola za Marekani bilioni tano kwa ajili ya kusaidia watoto wa Tanzania husuan wa kike.

"Kampuni hii inatoa somo kwa vijana wa Tanzania wanapoanzisha kampuni zao au wanaporithi wasiwaze kugawana mali bali kuendeleza. Vipo vikundi vinaanzishwa na wanapopata fedha wanagawanyika," alisisitiza.

Mwigulu aliitaja changamoto kubwa inayoikabili sekta hiyo kuwa ni elimu ndogo ya umuhimu wa bima na kutokuwapo kwa mtandao mkubwa.

Alisema wataendelea kuhamasisha Watanzania kutumia bima hizo ili kujikinga yanapotokea madhara mbalimbali.

"Tunaomba Watanzania wachukulie bima ni jambo muhimu kwani hata mataifa mengine duniani yanakuwa kiuchumi kutokana na matumizi ya bima," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Alliance, Shaffin Jamal, alisema katika kipindi cha miaka 25 ya kampuni hiyo imepata mafanikio mbalimbali.

Alisema wamefikia mtaji wa Dola za Marekani bilioni 100 na kuongeza bidhaa mbalimbali katika matawi matano nchini.

Alisema kampuni hiyo imeruhusu matumizi ya teknolojia na kukuza ustawi licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali.

"Kujitolea kwa dhati kwa AICL kumefanya Soko la Tanzania kuaminiwa na kwamba uvumbuzi umesababisha kuanzishwa kwa bidhaa na huduma mbalimbali, ikiwa ni pamoja na bima ya kilimo na iliyopachikwa, programu za simu na huduma za WhatsApp kwa picha," alisema Jamal.

Pia, alisema kwa kutumia teknolojia ya kidijitali, AICL imeboresha huduma zake na kuwapa wateja urahisi zaidi, kasi na uwazi katika safari yao ya kutoa bima.



# Wanafunzi Simanjiro wanufaika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHULE mbili za msingi Naisinyai na Oloshonyokie za Kijiji cha Naisinyai wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wanafunzi wake wamenufaika na msaada wa vyakula na mafuta vilivyotolewa na kampuni ya uchimbaji madini ya Tanzanite Franone Mining and Gems LTD.

Msaada huo ni magunia 120 ya mahindi, magunia 20 ya maharage na ndoo 20 za lita 400 za mafuta ya kupikia, umetolewa na kampuni hiyo ya uchimbaji madini kwenye kitalu D na wamiliki wa kitalu C.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Naisinyai, Merika Makeseni, akizungumza jana kijijini hapo, alishukuru kampuni hiyo na kusema msaada huo umekuja kwa wakati mwafaka.

Merika alisema kwa moyo wa dhati na kwa niaba ya jamii nzima ya wana Naisinyai, aliwashukuru wakurugenzi na uongozi wa kampuni hiyo kwa msaada waliotoa kwa shule hizo.

"Kimsingi maeneo yetu kama yalivyo maeneo mengi ya nchi yetu, kwa miaka mitatu yamekumbana na changamoto ya ukosefu wa chakula, hali iliyotokana na mvua kuwa chache sababu ya nchi kukabiliana na mabadiliko makubwa ya tabia nchi," alisema Merika.

Alisema hali hiyo pia imesababisha mifugo mingi ambayo ni tegemeo kubwa kwa jamii ya wafugaji kufa na michache iliyobaki kudhoofu kiasi cha kutouzika kirahisi na kwa bei rafiki.

Alisema kutokana na hali hiyo, wakaamua kuwashirikisha wadau wa maendeleo kwa mwaka huu, walau wasaidie chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi, ambao kwa kawaida huchangiwa na wazazi.

"Niwashukuru viongozi wenzangu waliotupa ushirikiano katika hili ambao ni Mkuu wa Wilaya, Suleiman Serera, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Gracian Makota, Ofisa Tarafa, Moipo Dhulfa Laizer na Diwani wa Kata Taiko Laizer, kwa namna walivyojitoa kuhakikisha tunafanikisha hili," alisema.

Alisema ni ahadi yake na kamati za shule kuwa chakula hicho watakisimamia kukihifadhi na kuhakikisha kitatumika kwa lengo lililokusudiwa.

"Ni maombi yetu kwa Mungu wetu kuwabariki kampuni ya Franone Mining and Gems LTD na kuwajazilizia wale waliokitoa ili wasijutie wao kwa kutoa sadaka hii kubwa kwa watoto wetu," alisema Merika.

Mkuu wa Shule ya Msingi Naisinyai, Agnes Chang'endo na Makamu Mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, Tauta Siria, walishukuru kampuni ya Franone Mining and Gems LTD kwa msaada huo wa chakula cha wanafunzi hao na watahakikisha chakula hicho kinatumika ipasavyo kwa lengo husika lililokusudiwa.

Mmoja kati ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Oloshonyokie, James Loishiye alisema msaada huo wa chakula utakuwa kichocheo, kwa wao kuhudhuria masomo.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakifurika kutazama mwili wa aliyekuwa mmiliki wa Taasisi ya Baruti inayojishughulisha na kukopesha fedha kwa jamii, Robart Baruti, ambaye amekutwa amefariki dunia pembeni ya reli jana asubuhi, Mtaa wa Masimbani, Kata ya Masuguru akiwa na jeraha usoni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# IAA kuboresha mitaala ya elimu kuendana na mahitaji

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA), kwa mwaka huu wa fedha kimeweka mpango mkakati wa kuboresha mitaala ya elimu zaidi ya 30 ili iendane na mahitaji na matarajio ya jamii.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka, wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa ripoti ya mwaka wa fedha uliopita wa 2022/2023.

"Kuna zoezi linaendelea la kuboresha mitaala zaidi ya 30 kwa kuwa ukiitengeneza kila baada ya miaka mitano inakuwa imepitwa na muda hivyo ni lazima kufanyike maboresho," alisema Prof. Sedoyeka.

Alisema pia chuo hicho, kimefanikiwa kuongeza mapato kwa kufikia Shilingi bilioni 26 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 15 kutoka mwaka uliopita wa fedha.

Aidha, alisema kiasi hicho cha fedha kimetokana na ongezeko la wanafunzi ambao ni 13,716 pia kuna sababu nyingie mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa mitaala na kuongeza kampasi za Babati, Dodoma na Ruvuma.

Alisema mafanikio hayo yametokana na kuwapo kwa mazingira rafiki ya kujifunzia kwa wanafunzi na wingi wa wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne ambao wanajiunga na chuo hicho kwa ajili ya kusoma.

"Tumeongeza mitaala na kwa shahada kuna mitaala 24 na stashahada 14 sambamba na kuweka mazingira rafiki ya kujifunzia, mfano kwa kipindi hiki tumeweza kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoweza kukaa kwenye viti kwa awamu moja hadi kufikia 9,000, hivyo kwa siku wanaweza kupokea wanafunzi 20,000 wanapobadilishana awamu za kuingia darasani.

"Kadhalika tumejenga majengo makubwa ambayo yanaweza kuweka wanafunzi wengi, ikiwamo jengo jipya la faru ambalo lina uwezo wa kubeba wanafunzi 3,800," alisema.

Pia alisema wamejikita katika uboreshaji wa mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na kwa mwaka uliopita walipata wafanyakazi wapya 26, waliohamia 28 na 52 walioko kwenye mafunzo ya uzamili, tisa wako Shahada ya Umahiri na wanne wanasoma ngazi ya Stashahada ya Uzamili.

Vilevile alisema chuo hicho kimefikisha wafanyakazi 334 na kati ya hao walimu ni 232 na wafanyakazi wa kiufundi 102 na wamelenga kuboresha mawasiliano kati ya chuo na nje ya chuo.

Katika hatua nyingine, Prof. Sedoyeka, alitumia fursa hiyo kuishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukipatia chuo hicho fedha nyingi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi(HEET).

"Sisi kama chuo tumebahatika kupata fedha za mradi wa HEET, tumepangiwa kupewa Dola za Marekani milioni 21 na zitatumika kuboresha miundombinu kwenye kampasi za Arusha, Babati na kujenga kampasi mpya Songea," alisema.

Alisema kwa kampasi ya Arusha, fedha hizo zitatumika kujenga kituo kikubwa cha kimkakati cha ICT na kukamilisha ujenzi wa hosteli za wanafunzi.

## RC aagiza vifaa ujenzi wa shule kununuliwa kiwandani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi, kuhakikisha vifaa vyote vya ujenzi wa shule mpya ya wasichana kitaifa, inayojengwa wilayani humo vinanunuliwa kiwandani ili kupunguza gharama.

Aidha, aliagiza mradi huo ujengwe kwa kutumia mfumo wa "Force Account badala ya kutumia mkandarasi, ili fedha zilizotengwa zitoshe kukamilisha ujenzi huo.

Alitoa agizo hilo baada ya kutoridhishwa na taarifa iliyosomwa na Ofisa Manunuzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Godbless David ya gharama kubwa za ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kutoka kwa wazabuni waliokuwa wameomba kupeleka vifaa katika mradi huo, ambao gharama yake ni Sh. bilioni tatu fedha kutoka serikalini.

Mongella alisema hayo jana wilayani Longido wakati akikagua ujenzi wa shule hiyo ambao upo katika hatua za awali na kuagiza lori la halmashauri ya wilaya hiyo, lianze kupeleka mawe na mchanga eneo husika, badala ya kukodisha malori ya watu binafsi.

"Mkuu wa Wilaya ninakuagiza kuanzia sasa vifaa vyote vya ujenzi visinunuliwe kwa wazabuni, badala yake viagizwe viwandani moja kwa moja ili kupunguza gharama, kwa sababu fedha zipo ili mradi uweze kukamilika kwa kiwango kinachotakiwa na kwa wakati," alisema.


Pia alimwagiza mkuu huyo wa wilaya kuhakikisha miundombinu yote muhimu, ikiwamo maji na umeme inapelekwa kwenye eneo hilo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa stoo, ili kuharakisha shughuli za ujenzi huo ambao unatakiwa kukamilika Desemba mwishoni.

"Kesho jioni nitarudi hapa kukagua tena hali ya ujenzi nikifika nataka nikute umeme ukiwaka pamoja na huduma ya maji, haiwezekani mafundi wakae hapa wakati hakuna maji wala umeme. Huku ni kukwamishana, hakikisha huduma hizi zinafika hapa mara moja," alisema.

Kuhusu kamati ya ujenzi Mongella aliagiza mwenyekiti wake awe mwananchi wa kawaida, asiyekuwa na wadhifa kwenye vyama vya siasa au kwenye madhehebu ya dini kama mwongonzo unavyoelekeza.

Ng'umbi alisema amepokea maagizo yote yaliyotolewa na Mongella na kusema atasimamia kikamilifu mradi ili ukamilike kwa wakati, huku akiahidi kufanya kazi bega kwa bega na kamati zitakazoundwa kwa ajili ya kusimamia mradi huo.

Ofisa Elimu Mkoa wa Arusha, Abel Ntupwa alisema serikali kupitia Mradi wa Kuboresha Shule za Sekondari Nchini (SEQIP) imetoa Sh. bilioni tatu kuanzia Julai mwaka huu, lakini kumekuwa na hali ya kusuwa suwa katika utekelezaji wa mradi huo.





Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto) na viongozi wa mkoa wa Mara wakipata maelezo kuhusu kampuni ya Barrick inavyoweka mkazo katika utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji kutoka kwa Ofisa Mazingira wa Barrick North Mara, Samwel Ingram, walipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maadhimisho ya Siku ya Mara yaliyofanyika katika viwanja vya Sokoine wilayani Serengeti mwishoni mwa wiki. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# TASAF yatakiwa kuja na ubunifu malipo kwa wazee, wasiojiweza

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameuagiza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuja na ubunifu mpya wa namna ya kuwalipa wazee na wasiojiweza, ili kukomesha vitendo vya wizi vinavyofanywa na ndugu au watu wanaowasaidia kutoa fedha kwa njia za simu.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kupokea taarifa ya mpango wa TASAF Mkoa wa Geita, ikiwa ni mwendelezo wa ziara anayoifanya katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Simbachawene alisema ubunifu wa kutoa malipo kwa simu ulilenga kupunguza gharama za uendeshaji lakini wamebaini tatizo la fedha hizo kutowafikia walengwa kutokana na wao kutokuwa na ubunifu au uwezo wa kutumia simu.

Simbachawene alisema: "Tuangalie upya namna tunavyowalipa hawa wazee ili tuwaondolee hili tatizo la kuibiwa. Najua mna mifumo yenu wakati mkitaka kuiboresha basi angalieni njia bora itakayo wawezesha wapate fedha hizi." Kuhusu fedha zinazotolewa kwa walengwa wasio na sifa, Simbachawene aliagiza kusitishwa kwa fedha hizo mara moja na badala yake zipangiwe kazi nyingine wakati wakisubiri kupata walengwa wenye sifa.

Naye Katibu Tawala Msaidizi (Mipango na Uratibu), Deodatus Kayango, alisema TASAF kwa Mkoa wa Geita inahudumia kaya 46,749 zenye walengwa 220,666 ambapo kwa kipindi cha pili cha awamu ya tatu zaidi ya Sh.milioni 35.4 zimelipwa kwa walengwa.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2021-2023 Mkoa wa Geita ulipokea Sh.bilioni 8.09 kwa ajili ya miradi ya kuondoa umaskini ambayo ni ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya, miradi ya ajira za muda pamoja na miradi ya vikundi kwa walengwa.

Kayango alisema mpango huo umewezesha wanafunzi wa msingi na sekondari kupata mahitaji ya watoto kwa ajili ya kuendelea na masomo pamoja na kuwezesha watoto chini ya mikaa mitano kupelekwa kliniki.

Alitaja mafanikio mengine ni walengwa kumudu kupata mahitaji ya msingi ikiwamo kumudu kupata milo miwili kwa siku kutoka kwenye mlo mmoja waliokuwa wakipata awali pamoja na kufanikiwa kuezeka nyumba kwa bati kutoka nyumba za nyasi zilizokuwapo.

# TASAC yataja chanzo kukithiri ajali majini

**Na Restuta Damian,** KAGERA

WAKALA wa Meli Nchini (TASAC) Mkoa wa Kagera umesema sababu za kutokea ajali za mara kwa mara majini hususani katika Ziwa Victoria ni pamoja na uendeshaji wa mazoea wa vyombo hivyo unaoendekezwa na baadhi ya manahodha.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Mfawidhi wa TASAC Mkoa wa Kagera, Mzee Mvihanga wakati akiongea na Nipashe juu ya suala la usalama wa vyombo vya majini.

Mvihanga alisema waendeshaji wa vyombo hivyo wapo ambao hawafahamu sheria na taratibu za kuchukua tahadhari za mazingira ya hatari endapo kuna upepo au mvua inaponyesha, kwamba wanatakiwa wasubiri kwanza ndipo kuendelea na safari zao.

Alisema zipo shughuli zinazofanywa nyakati za usiku ambazo zinahusisha wavuvi wanaotega samaki bila kuwa na viashiria mwanga ambacho kitamsaidia mwingine kuona mbele yake ili akwepe kugongana.

Kadhalika, alitaja ulevi na kutokuzingatia taratibu za kuendesha vifaa hivyo katika kipindi cha mvua kuwa ni miongoni mwa sababu za kutokea kwa ajali za kugongana na pia kuzama majini.

Alisema ipo haja ya wavuvi na waendesha vyombo vya usafiri kuwa na elimu inayotolewa na chuo cha baharia angalau kwa ngazi ya cheti ili imsaidie kujua sheria na matumizi ya muda sahihi wa kuendesha vyombo hivyo.

Alisema mbali na (TASAC) kutoa elimu ya mara kwa mara yenye utambuzi wa madhara ya kuendesha vyombo hivyo nyakati zinazoweza kusababisha ajali lakini bado mapokeo yake hayazingatiwi kwa usahihi.

Alisema kwa mwaka 2022 zilitokea ajali sita ikiwa tatu zilizohusisha vyombo vidogo vinavyofanya shughuli za uvuvi na zingine zilitokea kwa kuteleza na kutumbukia majini.

# Halmashauri Msalala yakamilisha ujenzi wa majengo makazi mapya

**Na Neema Sawaka,** MSALALA

HALMASHAURI ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga imekamilisha ujenzi wa majengo yake mapya eneo la Izengabatogilwe yaliyogharimu Sh. bilioni 4.5, wanatarajia kuhamia Oktoba mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba katika kikao cha kawaida cha kila mwezi kilichofanyika kwenye halmashauri hiyo.

"Tunashukuru kwa kupatiwa fedha kwa ajili ya kumalizia jengo la utawala, ikiwa ni pamoja na matumizi mengine kama ununuzi wa samani za ofisi, miundombinu ya umeme, maji, TEHAMA na marekebisho madogo kwani Sh.bilioni 4.5 hizo ziliongeza kasi ya ujenzi huu," alisema Katimba.

Aidha, alieleza kuwa katika majengo waliyokuwa wakiyatumia siyo makazi ya kudumu na tayari majengo mapya yamekamilika na kwa ubora unaokidhi viwango. Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, alisema baraza hilo limeridhishwa na kazi ya ujenzi huo akisema umekidhi vigezo vyote walivyokuwa wameweka kwenye nafasi hiyo.

Mweka hazina wa Halmashauri hiyo, Gordon Dinda, alisema katika kipindi cha Julai Mosi hadi Agosti 31, halmashauri hilo ilikusanya Sh.bilioni 1.5 sawa na asilimia 27 ya lengo la kukusanya Sh.bilioni 5.7 kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Naye Diwani wa Kata ya Ikinda, Matrida Msoma, alisema, wataalamu wa halmashauri hiyo wanapaswa kutumia mbinu mbalimbali kuhakikisha halmashauri hiyo inaongeza makusanyo.

# Wakazi wapewa angalizo mradi wa maji Butimba

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI mkoani Mwanza waaswa kuchemsha maji ya kunywa katika kipindi cha majaribio ya Mradi wa Maji Butimba ili kujinusuru na magonjwa mbalimbali. Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Neli Msuya, wakati akiwasilisha taarifa ya mradi na mipango ya uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Jiji hilo.

Alisema baada ya saa chache wananchi wa Sahwa, Igoma, Kishili, Kisesa na Nyamhongolo watakuwa wamefikiwa na maji, hivyo wanatakiwa kukumbushwa kwamba bado mamlaka iko katika majaribio, hivyo wanapaswa kuchemsha maji hayo.

Alisema huduma itaendelea kuimarika kwa wakazi wa Nyegezi, Luchelele, Buhongwa, Buswelu na Butimba kadri pampu zitakavyokuwa zinawashwa na uzalishaji wa maji kuongezeka. Mradi huo wa unaojengwa kwa Sh. bilioni 70, ni mbadala wa chanzo cha Caprpoint ambacho uzalishaji wake kwa siku ulikuwa ni lita milioni 90.

Alisema maji kutoka chanzo hicho yataingizwa katika mtandao mpya wa mabomba, hivyo wamejipanga kufanya marekebisho ya mabomba ya zamani ili kupunguza upotevu na kuondoa mabomba madogo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, akiwasha moja kati ya pampu za mitambo hiyo na kuanza rasmi majaribio alisema kukamilika kwa mradi huo ni pigo na habari mbaya kwa wapinzani wa serikali waliotarajia mradi kutokamilika.

Mbunge wa Ilemela, Angelina Mabula, alisema tatizo kubwa ilikuwa ni maji haikuwa rahisi kuwaeleza wananchi waishio kando ya Ziwa Victoria kukosa maji wakati yanafika hadi Tabora.

Naye Mbunge wa Nyamagana, Stansalu Mabula, alisema wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015 na 2020 kilio cha Nyamagana kilikuwa maji, hivyo alimshukuru Rais Samia Hassan kwa moyo wake wa dhati wa kuwezesha wananchi kupata maji kwa kutekeleza ahadi yake ya kuhakikisha mradi wa Butimba unakamilika.

Nipashe
Spotika



MECHI 3 HATUA YA MAKUNDI UEFA ZINAZOSUBIRIWA ZAIDI 12 - 13






# SABABU 5 KWA NINI MESSI ATAMSHINDA HAALAND MBIO BALLON D'OR 2023

**NYON, Uswisi**

MSHINDI wa Ballon d'Or 2023 atatangazwa Oktoba 30. Uchezaji wa wanasoka kutoka kote ulimwenguni katika msimu wa 2022-23, unazingatiwa kuwania tuzo hiyo. Jarida la France Football wiki mbili zilizopita lilitoa orodha ya wachezaji 30 walioteuliwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or kabla ya wiki iliyopita mchujo kufanyika na kubaki 12.

Majina mawili ambayo yanaongoza orodha hiyo ni Lionel Messi na Erling Haaland. Wachezaji hao wawili walikuwa katika hali nzuri msimu wa 2022-23.

Wakati Messi, ambaye sasa ana umri wa miaka 36, ameingia kwenye kinyang'anyiro cha maisha yake ya soka, Haaland ana umri wa miaka 23 tu na anaanza kile kinachotarajiwa kuwa utukufu.

Mashabiki na wadadisi wanaendelea kugawanyika kuhusu nani anafaa kushinda tuzo ya Ballon d'Or 2023.

Lakini hapa, tunaangalia sababu tano kwa nini Messi yuko mbele sana ya Haaland katika mbio za kushinda tuzo ya Ballon d'Or 2023.

**#5 Mchango wa Messi msimu uliopita**

Mchezaji huyo mashuhuri wa Argentina amekuwa na mchango mkubwa katika ulimwengu wa soka kwa mwaka uliopita. Alivunja rekodi ya mtandao wa kijamii baada ya kushinda Kombe la Dunia alipochapisha picha akiwa na wachezaji wenzake wa Argentina. Hadi sasa chapisho lake ndio lililopendwa (like) zaidi kwenye Instagram kwa zaidi ya milioni 75.6.

Hiyo ni kiasi cha ushawishi aliona Messi kwa kiwango cha kimataifa. Zaidi ya hayo, uamuzi wa Messi kutokwenda Saudi Arabia na badala yake kujiunga na Inter Miami ya Ligi Kuu Marekani (MLS), umeongeza umaarufu wa "soka" nchini humo.

Ameichukua MLS kwa kasi na amefunga mabao 11 na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 11 katika mashindano yote akiwa na Inter Miami.

**#4 Messi alishinda Kombe la Dunia 2022**

Bila shaka, Kombe la Dunia linashikilia umuhimu mkubwa kama taji la kifahari zaidi katika kisoka. Mwishoni mwa mwaka 2022, Messi aliiongoza Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia, akionesha ujuzi wake wa kipekee kama mchezaji bora wa La 'Albiceleste' hao wakati wa mashindano yote.

Alipata bao katika kila mechi ya hatua ya mtoano ya Argentina, ikiwa ni pamoja na jozi za mabao katika fainali dhidi ya Ufaransa. Messi alijitokeza katika nyakati muhimu kwa timu yake na alitunukiwa tuzo ya Mpira wa Dhahabu kwenye Kombe la Dunia.

Kwa bahati mbaya kwa Haaland, Norway ilishindwa hata kufuzu Kombe la Dunia.

**#3 Messi alifanya vema Paris Saint-Germain**

Mbali na kuwa kinara wa Argentina katika mzunguko wa kimataifa, Messi alikuwa katika kiwango kizuri katika klabu yake ya zamani ya Paris Saint-Germain pia msimu wa 2022-23. Akiwa na nafasi ya kujiondoa zaidi ya ile tuliyozoea kumuona, alionesha uwezo wake wa kipekee wa kucheza na kufunga mabao.

Katika mechi 41 kwenye mashindano yote akiwa na Paris Sain-Germain, Messi alifunga mabao 21 na kutoa asisti 20. Michango yake ilikuwa muhimu kwa PSG kushinda taji la Ligue 1.

#2 Haaland alitegemea zaidi wachezaji wenzake

Haaland alifunga mabao 52 na kutoa pasi za mabao 11 katika mechi 53 kwenye michuano yote msimu uliopita na kuiwezesha Manchester City kutwaa mataji matatu. Lakini inafaa kuzingatia kwamba hakufanya yote peke yake.

Manchester City wana moja ya kikosi bora zaidi duniani na mshambuliaji huyo wa Norway anaungwa mkono na mafundi wa kiwango cha kimataifa uwanjani. Kwa mfano, mmoja wa wachezaji wakuu wa City ni Kevin De Bruyne, ambaye alisajili pasi nyingi za mabao 32 katika mashindano yote msimu uliopita.

Kwa kuongezea, watu kama Jack Grealish, Phil Foden, Ilkay Gundogan na Bernardo Silva walihakikisha kuwa Haaland hajawahi kuteseka kutokana na uhaba wa huduma. Ushindi wa mataji matatu wa City ulikuwa zaidi ya juhudi za pamoja kuliko kuchungulia takwimu za Haaland kutoka msimu uliopita.

**#1 Haaland hakufunga katika fainali zote**

Licha ya mafanikio yake yote katika msimu wa 2022-23, Haaland amekosolewa kwa kutoweza kujitokeza katika hali ngumu. Mshambuliaji huyo wa Norway alishindwa kufunga bao katika fainali za Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia alishindwa kufunga katika mechi mbili za nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya City na Real Madrid. Haaland alifunga bao lingine katika nusu fainali ya Kombe la FA ya City dhidi ya Sheffield United. Tabia hii ya kutokuwa na mchango katika michezo muhimu inaweza kumgharimu kwenye kinyang'anyiro hicho cha kuwania tuzo ya Ballon d'Or 2023.

Kwa upande mwingine, Messi alijitoa mno wakati akielekea kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia akiwa na Argentina kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

## ISIKUPITE

WACHEZAJI sita waliofunga mabao mengi ya mpira uliokufa (free-kick), katika historia ya soka duniani, #1 Juninho Pernambucano (mabao 77), #2 Pele (mabao 70), #3 Victor Legrotaglie (mabao 66), #3 Ronaldinho (mabao 66), #5 Lionel Messi (mabao 65 ) na #5 David Beckham (mabao 65).



## Extra Time



Mabingwa wa Ligi ya Mabindwa Ulaya msimu uliopita, Machester City, wakifurahia kwa pamoja baada ya kukabidhiwa kombe. **PICHA: MTANDAO**

# MECHI 3 HATUA YA MAKUNDI UEFA ZINAZOSUBIRIWA ZAIDI

**LONDON, England**

LIGI ya Mabingwa Ulaya imerejea, droo iliyochezeshwa hivi karibuni ilikuja na mambo mengi ya kustaajabisha huku klabu 32 zikijaribu kupambana kuwania taji linaloshikiliwa na Manchester City.

Wakati droo hiyo imekuwa nzuri zaidi kwa Man City, Barcelona na Atletico Madrid, hilo haliwezi kusemwa kuhusu Paris Saint Germain, AC Milan na Manchester United.

Wakati Kundi F litajazwa na mizozo ya kiofisi, vikundi vingine haviko nyuma linapokuja suala la midomo, Bayern Munich na Arsenal zitalazimika kuepuka misukosuko inayoweza kutokea.

Makala haya yanaangalia mechi tatu zinazosubiriwa zaidi za hatua ya makundi ya UEFA msimu huu, twende sasa...

### #3. Napoli dhidi ya Real Madrid

Uwapo wa Napoli na Real Madrid huenda ukafanya Kundi C kuwa upande mmoja, vita halisi itafanyika kati ya wababe hao wawili kuwania nafasi ya kwanza kwenye kundi hilo.

Union Berlin na Braga huenda zikawa tishio kwa mabingwa watetezi wa Italia na mabingwa mara 14 wa Ulaya. Hata hivyo, Napoli na Madrid zitakuwa zikijaribu kutinga kileleni ili kuepukana na upinzani mkali katika hatua ya 16-bora.

Napoli waliepuka kukabiliana na Real Madrid msimu uliopita kwa kumaliza wa kwanza Kundi A mbele ya Liverpool. Kwa hiyo, 'Wekundu' hao walilazimika kukabiliana na wababe hao wa Hispania ambao hatimaye waliwatupa nje ya mashindano.

Wakati huo huo, Real pia watajaribu kukwepa kumaliza mbele ya Napoli. 'Los Blancos' hao tayari wanauguza majeraha makubwa kutokana na kukosekana muda mrefu kwa Thibaut Courtois na Eder Militao. Kwa hiyo, wataonekana kuwa timu iliyopanda daraja katika hatua ya 16-bora.

Napoli na Real Madrid zote zimeanza msimu kwa ushindi mfululizo. Kwa hiyo, itakuwa ya kufurahisha kuwaona wakipambana kwenye hatua kubwa zaidi ya mpira wa miguu.

Mchezo utakaochezwa Naples utakuwa na jukumu kubwa katika kuamua matokeo ya kundi. Msimu uliopita, Napoli iliifunga Liverpool mabao 4-1 katika safari yao ya kutinga hatua ya makundi. Itakuwa ya kuvutia kuona jinsi watakavyocheza dhidi ya klabu iliyofanikiwa zaidi kwenye mashindano hayo.

### #2. AC Milan dhidi ya Paris Saint Germain

Kundi F huenda ndilo pekee ambalo timu zote nne zinaweza kutwaa nafasi mbili za juu. Hata hivyo, mchezo ambao utakuwa na umuhimu zaidi kwa michezo mingine yote utachezwa San Siro kati ya AC Milan na PSG.

PSG wanapewa nafasi kubwa ya kufuzu hatua ya 16-bora wakiwa vinara wa msimamo kwa sababu ya uwapo wa Kylian Mbappe na msisitizo wa PSG wa kujenga timu chini ya Kocha mpya, Luis Enrique. Lakini linapokuja suala la Ligi ya Mabingwa Ulaya AC Milan si wazembe pia.

Christian Pulisic, Ruben Loftus-Cheek, Yunus Musah, na Samuel Chukwueze wote ni nyongeza nzuri kwa timu iliyofika nusu fainali msimu uliopita. Maendeleo yao chini ya Stefano Pioli yamekuwa ya polepole na thabiti na watakuwa tishio kwa kundi lingine.

Mtihani mgumu zaidi wa PSG ugenini utakuja dhidi ya AC Milan. Wachezaji hao wa Paris watakuwa wakiwa baada ya kuondoka kwa Lionel Messi na Neymar. Kwa hiyo, safari ya San Siro itathibitisha kuwa mtihani wa kwa Luis Enrique na kikosi chake cha vijana.

Kushindwa katika mchezo huu kunaweza kusababisha maafa kwa pande zote mbili, haswa AC Milan. 'The Rossoneri' hao watahitaji kushinda dhidi ya PSG nyumbani kwao ikiwa wanataka kuongoza kundi.

Klabu nyingine kubwa katika kundi Borussia Dortmund na Newcastle United pia si za kubeza. Timu zote mbili zitahitaji kuongoza kundi lao ili kuepuka kukutana na mpinzani wa taji katika hatua ya 16-bora.

### #1. Manchester United dhidi ya Bayern Munich

Manchester United na Bayern Munich zote ni wafalme wa Ulaya. Vinara hao wawili wa Ulaya wanashiriki kutwaa mataji tisa ya Ligi ya Mabingwa baina yao (Bayern mara sita, United mara tatu) na hawatarajii hali ya wastani katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, timu hizo mbili haziko karibu na viwango walivyoweka wakati wa mbio zao za kushinda mataji barani Ulaya kwa miaka mingi. Wakati United wameshindwa kufika fainali ya shindano hilo kwa zaidi ya muongo mmoja, Bayern wameshindwa kuiga kiwango chao cha msimu wa 2019-20.

Lakini, Bayern wanakaribia zaidi kufikia viwango vilivyowekwa na Manchester City msimu uliopita. Uhamisho wao wa majira ya joto wa Harry Kane umewapandisha hadhi ya kuwa miongoni mwa wachezaji watatu wanaowania taji hilo pamoja na Real Madrid na Manchester City.

Kwa upande mwingine, kiwango duni cha Manchester United ugenini dhidi ya vigogo hao kimekuwa kikiumiza kichwa sana kwa Erik ten Hag. 'Mashetani Wekundu' hao walishindwa kushinda ugenini dhidi ya wababe hao wa jadi msimu uliopita. Mbali na hilo, walipoteza ugenini kwa Spurs msimu huu pia.

Kwa hiyo, ukweli kwamba Mholanzi huyo atalazimika kusafiri Munich kumenyana na Bayern kunamnyima usingizi. Copenhagen hawakufungwa nyumbani dhidi ya City, Dortmund, na Sevilla msimu uliopita. Galatasaray si wakubeza sana. Kwa hiyo, kimsingi, hakuna timu yoyote kwenye kundi lao itakafungwa kirahisi.

Kwa hiyo, mchezo dhidi ya Bayern pale Old Trafford utakuwa na jukumu muhimu katika kampeni ya United ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mbali na hilo, mchezo huo utakaopigwa Old Trafford pia utakuwa mtihani mgumu zaidi kwa Wajerumani hao katika hatua ya makundi. Chochote chini ya pointi tatu kinaweza kuwa na sauti kubwa kwenye kampeni za klabu zote za Ulaya.

## Nukuu

"Ninajiamini, ninaamini. Najua bado ninaweza kuboresha mengi, bado ni mdogo. Lakini ndio, nadhani nina nafasi mwaka huu," **Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland akiamini kwamba yuko kwenye nafasi nzuri ya kushinda Ballon d'Or 2023 mbele ya Lionel Messi. Wachezaji hao wawili ndio wanaopewa nafasi kubwa kushinda tuzo hiyo mwaka huu.**



"Familia yangu ilinihimiza kuja Saudi Arabia, hasa kwa vile ni nchi ya Kiislamu. Mama yangu alifurahi sana na akasisitiza hilo nikaichagua Al-Nassr," **Sadio Mane akigusia jukumu la familia yake katika uamuzi wake wa kuelekea Saudi Pro League na kujiunga na Al-Nassr msimu huu wa majira ya joto.**



"Cristiano kwangu, unajua, matokeo gani, ni mwenye nidhamu sana. Mimi ni mtu mwenye nidhamu sana, unajua na kuwa na mafanikio ya aina hiyo na kuwa na nidhamu wakati huo huo ni kitu ambacho nimekuwa nacho siku zote. Mara zote ninavutiwa naye. Ninawapenda wote wawili. Lakini mimi binafsi, mimi ni mvulana wa Ronaldo," **Mwanamuziki wa Nigeria, Davido akichagua Cristiano Ronaldo mbele ya Lionel Messi alipokuwa akitoa maoni yake kuhusu mjadala mkuu wa soka.**





Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama (mbele), akishangilia pamoja na wachezaji wenzake, baada ya kuifungia timu yake bao la pili la kusawazisha dhidi ya Power Dynamos kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola nchini Zambia juzi. Kushoto ni Luis Miquissone, kulia ni Jonh Bocco na nyuma ni Jean Baleke. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# USIYOJUA SIMBA, YANGA ZIKICHEZA CAF UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU kubwa na kongwe zenye mashabiki wengi nchini, Simba na Yanga juzi zilikuwa kwenye nchi tofauti kuiwasilisha Tanzania katika michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika, kila moja ikiwania kuingia hatua ya makundi.

Mabingwa wa Tanzania Bara Yanga walikuwa kwenye Uwanja wa Kigali Pele, Nyamirambo nchini Rwanda kucheza dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan ilioutumia uwanja kama wa nyumbani kutokana na kuwapo kwa machafuko nchini kwao, na wageni wakifanikiwa kushinda mabao 2-0.

Watani zao wa jadi, Simba walikuwa kilometa nyingi katika mji wa Ndola nchini Zambia kucheza na Mabingwa wa nchini hiyo, Power Dyanamos, mechi ikipigwa Uwanja wa Levy Mwanawasa. Katika mechi hiyo, Simba ililazimisha sare ya mabao 2-2.

Baada ya mechi hizo timu zote sasa zitacheza mechi za marudiano jijini Dar es Salaam, Uwanja wa Azam Complex kwa siku tofauti, Yanga ikitarajiwa kukipiga Septemba 30 dhidi ya Al Merrikh, na kesho yake Oktoba Mosi, mwaka huu Simba itamalizana na Power Dyanamos.

Yanga ambayo inawania kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika mara ya kwanza baada ya miaka 24, inatakiwa kushinda, kutoa sare au kutoruhusu kufungwa zaidi ya bao moja katika mechi hiyo, huku Simba ambayo imekuwa sasa ni kama utamaduni wake kutinga hatua hiyo, kupata ushindi, au sare yoyote, lakini haitakiwa kupoteza hata kwa bao 1-0.

Haya ni baadhi ya matukio, rekodi ya takwimu za kukumbukwa katika mechi zote hizo mbili zilizochezwa Rwanda na Zambia.

**1. Rekodi ya kucheza muda mmoja**

Kwa mara ya kwanza imeshuhudiwa Simba na Yanga zikicheza muda mmoja katika mechi yoyote ya michuano. Haijawahi kushuhudiwa hilo kwani hata kama itatokea zikicheza siku moja basi muda utakuwa tofauti.

Katika mechi za Ligi Kuu huzitofautisha siku, moja ikicheza leo nyingine itacheza kesho na kama nyingine ikicheza saa 10:00 jioni, basi moja itacheza usiku. Juzi kwenye michuano hiyo hiyo, timu hizo zilicheza muda mmoja kitu ambacho ni nadra sana kutokea kama vile kupatwa kwa mwezi au jua.

Kwenye vibanda umiza ililazimika kuwekwa TV mbili ili mashabiki wa pande zote waangalie mechi, lakini pia ilikuwa ni purukushani, hekaheka na kuvutana mashati sehemu ambazo TV ni moja na mashabiki kulazimika kuangalia kwa zamu, dakika 15 kumi na tano.

**2. Yanga kushinda mara saba ugenini**

Kwa sasa si stori tena Yanga kushinda ugenini katika mechi za kimataifa kwani juzi imefanya hivyo kwa mara ya saba tangu msimu uliopita.

Pamoja na kwamba baadhi ya mechi ikiwamo juzi haikuwa ugenini halisi kwa timu inazocheza nazo, lakini kikanuni inahesabika hivyo.

Msimu huu kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa imeshinda mara mbili dhidi ya Ali Sabieh ASAS ya Djibouti mabao 2-0 na Al Merrikh idadi kama hiyo ya mabao.

Msimu uliopita katika mechi za Kombe la Shirikisho, ilishinda ugenini mabao 4-0 dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, 1-0 dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, mabao 2-0 dhidi ya Rivers United ya Nigeria, 2-1 dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini na bao 1-0 dhidi ya USMA Alger ya Algeria.

**3. Mzize kuendeleza kutupia**

Straika anayekuja juu wa Yanga, Clement Mzize, amefunga mabao mfululizo katika michuano hiyo, akiendeleza pale alipoishia kwenye mechi ya hatua ya awali dhidi ya ASAS.

Mzize alipachika bao dakika ya 78 likiwa ni la pili kwa timu yake, ikitoka na ushindi wa mabao 2-0 juzi.

Mechi ya mwisho kabla ya juzi, Agosti 26, alifunga bao dakika ya 68 katika mechi ambayo Yanga ikiiadhibu ASAS mabao 5-0 Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

4. Wazambia kuwabeba Wabongo

Katika mabao manne yaliyofungwa na timu za Simba na Yanga juzi kwenye michuano ya kimataifa, matatu yamefungwa na wachezaji raia wa Zambia.

Kenndy Musonda aliifungia Yanga bao la kwanza katika mechi hiyo akichangia ushindi wa mabao 2-0, huku Clatous Chama akifunga mabao mawili katika mechi ambayo Simba ilitoka sare ya mabao 2-2.

Ni bao moja tu limefungwa na Mtanzania, Mzize, hivyo wachezaji wao wa Kizambia kuwa na mchango mkubwa katika matokeo yaliyopatikana kwa timu hizo mbili kubwa za Bongo.

**5. Wazambia wote kutupia Zambia**

Rekodi nyingine ni kwamba mabao yote manne yaliyofungwa katika Uwanja wa Ndola Zambia kati ya Power Dynamos dhidi ya Simba yamefungwa na wachezaji wa Kizambia.

Wazambia Joshua Mutale na Cephas Mulombwa waliifungia Power Dynamos, huku Mzambia mwenzao, Chama akiifungia Simba mabao yote mawili.

## JE, WAJUA?



KAMA Simba itafanikiwa kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, katika droo ya kupanga makundi itakuwa Pot 2 endapo Al Ahly, Wydad, Mamelodi na Esperance nazo zitafuzu, lakini kama moja kati ya timu hizo nne haitafuzu basi Wekundu wa Msimbazi hao wataingia Pot 1. Hiyo ni kutokana na Raja Casablanca na Berkane ambazo katika viwango vya CAF zipo juu ya Simba kutokuwapo katika michuano hiyo msimu huu.





# TRA: Risiti utakayopewa iendane na gharama ya manunuzi yako

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Dodoma imewataka wananchi kujenga utaratibu wa kukagua gharama halisi za bidhaa walizonunua kwenye risiti wanazopewa na wafanyabiashara, ili kuepuka kutozwa faini ya asilimia 20 ya bidhaa husika.

Meneja wa TRA Mkoa wa Dodoma, Castro John, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye uzinduzi wa kampeni ya awamu ya pili ya tuwajibike yenye lengo la kuwakumbusha wafanyabiashara kuwajibika katika kutoa risiti halali za EFD kila wanapofanya mauzo ya bidhaa au huduma.

Alisema wakifanya hivyo itasaidia serikali kuingiza mapato na kuepusha udanganyifu unaofanywa na wafanyabiashara.

Alifafanua kuwa serikali inategemea mapato ya kodi katika kujiendesha na kuboresha huduma za jamii, hivyo ni muhimu kwa wanunuzi pia kudai risiti hizo na kuzikagua ili kujiridhisha uhalali wake ikiwamo kukidhi vigezo vyote muhimu kama tarehe na muda wa mauzo, jina la mnunuzi na gharama halisi hali itakayoepusha udanganyifu.

"Wafanyabiashara wanapaswa kuwajibika kutoa risiti halali bila kusubiri kushurutishwa, tukifanya hivyo tunaisaidia Serikali kutimiza malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo na kukuza uchumi, wafanyabiashara pia jitokezeni kulipa ushuru," alisema John.

Alifafanua kuhusu kampeni ya tuwajibike alisema njia watakazotumia kufanikisha kutoa elimu kwa wauzaji na wanunuzi kwa mitaa yote ya Dodoma na Wilaya ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa utoaji risiti halali za EFD na kuwachukulia hatua wauzaji wasio fuata sheria.

Alisema: "Kwa wasiotoa au kudai risiti watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria kwa kutozwa faini ambayo itakuwa kubwa kati ya shilingi milioni 1.5 au asilimia 20 ya thamani ya bidhaa iliyouzwa, kwa mnunuzi àsiyedai risiti atatozwa faini ambayo itakuwa kubwa kati ya Sh. 30,000 au asilimia 20 ya Kodi aliyokwepa," alisema.

Meneja huyo alisema kampeni hiyo inalenga maeneo yote ya biashara ambapo mkazo zaidi utawekwa katika maeneo korofi ambayo ni usafirishaji wa vifurushi au vipeto vinavyokwenda mikoani kwa kutumia usafiri wa mabasi na maroli na eneo la pili ni maeneo ya wauzaji wa jumla na maduka makubwa.



Meneja Mpango wa Taifa wa Chanjo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Florian Tinuga, akitoa mafunzo kwa wanahabari jijini Dodoma ya kuwajengea uwezo wa kuwaelimisha na kuwahamasisha wazazi na walezi kujitokeza kuwapeleka watoto kupata chanjo ya polio ya matone itakayofanyika kuanzia Septemba 21 hadi 24 mwaka huu kwenye mikoa sita ikiwamo Katavi, Kigoma, Kagera, Mbeya, Rukwa na Songwe. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Kamati yaundwa kutokomeza ukatili wanawake, watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

TAASISI ya Social Action Trust Fund (SATF) inayoratibiwa na serikali imeunda kamati za mpango kazi wa taifa kwa ajili ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika kata 10 za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida. Akizungumza jana wakati wa kutoa mafunzo hayo kwa wajumbe walioteuliwa kuunda kamati hizo, Meneja Miradi wa taasisi hiyo, Nelson Rutabanzibwa, alisema SATF imekuwa ikiwawezesha watoto kwa kuwapeleka shuleni na kuhakikisha afya zao zinakuwa sawa kwa kuwapatia bima ya afya.

Alisema kamati hizo zitakuwa na wajumbe ambao ni viongozi kutoka idara mbalimbali za serikali, asasi za kiraia, viongozi wa dini, wawakilishi wa makundi ya watu wenye ulemavu, wanafunzi na wanawake ambapo wenyeviti wa kamati watakuwa ni maofisa watendaji kata.

Rutabanzibwa alisema kamati hizo zinawasaidia katika miradi yao kuhakikisha watoto wanabaki shuleni kwa sababu vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto vinawafanya washindwe kutimiza ndoto zao kutokana na kupewa mimba, ndoa za utotoni, huku wengine wakiingizwa kwenye ajira wakiwa na umri mdogo.

Alisema kwa Mkoa wa Singida kuna changamoto kubwa ya watoto kuacha shule kwani walianza na watoto 80 lakini hadi sasa wamebaki na watoto 78 baada ya watoto wawili kutoka kwenye mradi kutokana na sababu mbalimbali kama, mimba, utoro na masuala ya nidhamu.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Eva Myula, akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo aliwataka washiriki kuyatendea kazi hasa kutokana na unyeti wa masuala hayo ya ukatili ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa kwenye jamii.

Mratibu wa Shirika la Oblige for Valnerable Children Tanzania (OVCT), Benard Sungi, ambao wanafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi hiyo alisema kwa ushirika wao wameweza kufanya kazi katika kata nne za Ihanja, Lighwa, Isunna na Kituntu ambapo waliwabaini watoto 80 ambao walikuwa katika mazingira magumu ambao wamepata ufadhili wa masomo kupitia taasisi ya SATF.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ikungi, Mariam Mwandekile, alisema mafunzo hayo yamelenga kuzifikia kamati za MTAKUWWA katika kata 10 ambazo ni Puma, Kituntu, Ihanja, Issuna, Dung'unyi, Mtunduru, Sepuka, Makiungu, Mungaa na Lighwa. Alisema anaamini kuwa kamati hizo zitakapoanza kutekeleza majukumu na mikakati yao zinakwenda kumaliza kama siyo kupunguza kabisa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye maeneo yao.

# Watoto 3,250,598 kupatiwa chanjo ya polio, matone

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATOTO walio chini ya umri wa miaka nane mkoani hapa wanatarajiwa kupata chanjo ya polio na matone itakayofanyika Septemba mwaka huu.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Chanjo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Florian Tinuga, aliyasema hayo alipokuwa akitoa mafunzo kwa waaandishi wa Mkoa wa Dodoma kuhusu uhamasishaji katika kutoa taarifa sahihi za kampeni ya utoaji wa chanjo ya polio ya matone kwa watoto.

Alisema watoto hao ni kutoka mikoa sita ya Kigoma, Kagera, Katavi, Mbeya, Songwe na Rukwa ili kuwakinga na ugonjwa wa polio.

Dk. Tinuga alitaja mikoa hiyo idadi ya watoto watakaofikiwa kwenye kampeni hiyo ya kupatiwa chanjo ya polio ni pamoja na Mbeya watoto (614,345) Kagera (729,387) Kigoma (884,478) Katavi (227,862) Rukwa (391,882) na Songwe (402,644).

"Kazi ya utoaji chanjo inatarajiwa kuzifikia Halmashauri 37 zilizopo kwenye mikoa hiyo sita na litafanyika kuanzia Septemba 21 hadi 24 na tunaamini wazazi na walezi wenye watoto hao walio chini ya miaka minane watafikiwa na kupatiwa chanjo hiyo muhimu," alisema.

"Kwa upande wetu tumejipanga kuhakikisha utoaji wa chanjo hiyo unafanikisha kwa kufanya kampeni ya kuwafikia watoto hao nyumba hadi nyumba, mtoto hadi mtoto na tuna uhakika wazazi na walezi watatoa ushirikiano ikiwemo nyinyi wana habari kupitia taarifa zenu," alisema.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule aliwataka wazazi na walezi kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kazi hiyo kwa kuwapeleka watoto kwenye vituo vya afya kupatiwa chanjo hiyo muhimu ya matone ya polio.

Alisema kuwa utoaji wa chanjo hiyo utafanyika katika mikoa sita ni matumaini ya serikali kuwa wazazi na walezi wenye watoto walio chini ya miaka nane watawapeleka kwenye vituo vya afya na wale watakaokutwa majumbani watapata chanjo hiyo.

Senyamule alisema kwa mkoa wa Dodoma asilimia 100 ya watoto wanaostahili kupata chanjo hiyo wanapatiwa kwenye vituo vya afya kwa ajili ya kuwalinda na magonjwa ya kuambukiza.





# Serikali yatangaza kampeni kudhibiti kirusi cha polio

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MLIPUKO wa kirusi kipya cha polio kwenye mataifa jirani ikiwamo Malawi, umeiamsha serikali ambayo imetangaza kampeni maalumu ya chanjo kwa watoto wote wenye umri wa chini ya miaka nane kwa lengo la kukabiliana na kirusi hicho.

Mwishoni mwa wiki Kamati ya Msingi ya Afya ya Mkoa wa Mbeya ilifanya kikao maalumu na maofisa kutoka Wizara ya Afya ambao wataungana na kamati ya chanjo ya mkoa huo kutoa chanjo kwa watoto.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Ofisa Programu wa chanjo kutoka Wizara ya Afya, Zainab Nyamgumi alisema kampeni ya chanjo hiyo itafanyika ndani ya siku nne kuanzia Septemba 21 mpaka 24 mwaka huu.

Alisema aina mpya ya kirusi hicho cha polio ni hatari zaidi kuliko vilivyowahi kutokea na hivyo akasisitiza kuwa chanjo hiyo lazima itolewe kwa watoto wote ambao wana umri wa chini ya miaka nane.

Alisema kwanza mwenye kirusi hicho alipatikana hivi karibuni mkoani Rukwa na kwamba ilibainika kuwa alipata maambukizi hayo kutoka Burundi na hivyo wakaamua kuanza kampeni hiyo katika mikoa yote ya pembezoni.

"Kwa kuanzia kampeni hii itafanyika katika mikoa ya pembezoni ambayo ni Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma na Kagera, timu za wataalamu zitapita katika wilaya zote na kuhakikisha watoto wote wanachanjwa," alisema Zainab.

Alisema wamepanga kutoa chanjo hiyo kwa kupita nyumba kwa nyumba ili kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuchanjwa wanafikiwa na chanjo hiyo.

Alisema ugonjwa wa polio hauna tiba yoyote isipokuwa unakingwa kwa njia ya chanjo, huku akisisitiza kuwa madhara ya ugonjwa huo ni kusababisha ulemavu kwa watoto na kifo.

Naye Asteria Shirima ambaye pia ni ofisa kutoka Wizara ya Afya alisema kutokana na mwingiliano wa watu kwenye mikoa hiyo, watawachanja hata watoto wanaoingia nchini kutoka kwenye mataifa jirani ili na wao wawe salama.

Alisema kutokana na hali hiyo, Mkoa wa Mbeya umeongezewa chanjo zaidi ya 100,000 ikilinganishwa na lengo uliopangiwa ili kuhakikisha na watoto wanaotoka nje ya nchi wanachanjwa. Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Elizabeth Nyema, alisema lengo la mkoa huo ni kuchanja watoto 614,346 ambao wana umri wa chini ya miaka nane na kwamba kwa sasa serikali imeongeza umri wa kuchanja kutoka chini ya miaka mitano mpaka nane.

Alisema wamepanga kutoa chanjo hiyo katika maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu ikiwamo makanisani na misikitini, kwenye vituo vya kulelea watoto yatima, vituo vya mabasi, kwenye masoko na maeneo mengine ambayo watoto wanapatikana.

Alisema wataalamu zaidi ya 1000 watasambazwa katika maeneo yote ya mkoa huo ili kuhakikisha watoto wote wanafikiwa na huduma hiyo ambayo inatolewa bila malipo.



Katibu Tawala wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Wakili Mariam Msengi (kulia), akishiriki kuondoa taka ngumu katika Mwalo wa Butuja juzi, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kwa kushirikiana na Shirika la Synergistic Globe na Mtandao wa Waandishi wa Habari TAJOWEP. Kulia ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Butuja, Kitonge Mwita. **PICHA: VITUS AUDAX**

# M/kiti CCM awashukia watumishi wasiowajali wagonjwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga, amesema kuna baadhi ya watumishi katika kada ya afya wamekuwa hawajali kuwahudumia wananchi, badala yake wanatumia muda mwingi kuzungumza na simu.

Sanga aliyasema hayo wakati alifungua kikao cha Halmashauri Kuu CCM Mkoa wa Njombe na kusema Rais Samia Suluhu Hassan amejenga vituo vya afya, hospitali, zahanati lengo likiwa ni kusogeza huduma kwa wakati.

"Baadhi ya watumishi wakati fulani wamekuwa wakizungumza na simu hawawajali kuwahudumia wananchi, kwa hiyo wananchi hawa wanakuja kutuambia sisi kama chama wanakasirika sana, kwa hiyo leo tumeona ni vizuri tumuagize Mkuu wa Mkoa ahakikishe anaenda kusimamia jambo hili, nia ya mama ni kujenga vituo ili wananchi wahudumiwe," alisema Sanga.

Aidha, alimpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, kwa hatua ya kukamata mtandao wa watu ambao walikuwa wakijihusisha na suala la ujambazi.

"Baada ya kupata taarifa ya ujambazi tulimwagiza na akasimamia vema, kikamilifu lakini vile vile tunawakuu wetu wa wilaya nao wanasikiliza maagizo ili kuweza kutatua kero katika mkoa wetu. Tunamwagiza tena Mkuu wa Mkoa kuhakikisha anasimamia vema katika mkoa, anatatua kero kwa wakati ili wananchi waweze kuishi kwa amani," alisema Sanga.

Mwenyekiti huyo pia aliagiza kuhakikisha kwamba mbolea inafika kwa wakati na kwenda kwa wananchi sambamba na kuuzwa kwa bei elekezi ambayo serikali imeelekeza.

"Na tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anawapenda Watanzania wakiwemo wa Mkoa wa Njombe kwa kutoa hela nyingi za ruzuku lakini vile vile tunampongeza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ambaye ndiye anasimamia wizara hii na timu yake ya wataalamu," alisema Sanga.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema hivi karibuni mkoani humo kulikuwa na changamoto ya matukio ya uhalifu.

"Majambazi na wezi ni ndugu zetu, ni marafiki zetu pia ni wanafamilia. Kwenye suala la uhalifu serikali kwenye vyombo vyetu tutatenda haki sasa haki itatafsiriwa katika namna nyingi lazima mkoa ulindwe, tuliwaambia wafanyabiashara wa Mkoa wa Njombe wafanye biashara saa 24," alisema na kuongeza:

"Hatuwezi kuwa na watu wanafanya biashara kwenye maduka ya pesa alafu kuna mtu anakaa kwenda kuvamia au kuvizia watu kwenye maduka hayo, hatuwezi kuvumilia jambo la kijinga namna hiyo," alisema.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema wananchi hasa wa maeneo ya pembezoni wanakabiliwa na changamoto ya kupanda kwa bei mafuta ya dizeli na petroli.

# Mwimbaji wa nyimbo za injili mbaroni tuhuma uchochezi

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

MWIMBAJI wa nyimbo za injili, Sifa Bujune (25) mkazi wa Isyesye jijini Mbeya, anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kuimba nyimbo zinazodaiwa kuwa na maudhui ya uchochezi na kusambaza katika mitandao ya kijamii.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema mwimbaji huyo alisambaza wimbo huo kwenye mitandao ya kijamii ikiwamo Youtube.

Alisema jeshi hilo linaendelea kumhoji mwimbaji huyo kabla ya kuchukua hatua zingine zikiwamo za kisheria kutokana na maudhui hayo ambayo hata hivyo hakuyataja.

"Uchunguzi zaidi unaendelea ili kupata taarifa zaidi zinazomhusu msanii huyu, tukishakamilisha tutamfikisha mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria," alisema Kamanda Kuzaga.

Kwa zaidi ya wiki mbili sasa vipande vya wimbo wa msanii huyo vinavyosadikika kuwa ndivyo vilivyomweka matatani vilikuwa vinazunguka mitandaoni.

Moja ya vionjo vya wimbo huo vinasema 'bandari inauzwa, wananchi tukilalamika hatusikilizwi kwa sababu mnatuona nyani,' 'Ngorongoro ndugu zetu wanahamishwa kwa nguvu, hii ni kwa sababu mnatuona nyani'.

Vionjo vingine alivyoviimba binti huyo ni kwamba 'Ina maana hao wageni wana thamani kwenye hii nchi kuliko wenyeji, mnatuona nyani,' 'kijana mdogo ameng'olewa meno na maaskari, hii ni kwa sababu mnatuona nyani'.

Pia anasema 'Masai ndugu wamelia kila kilio lakini hawasikilizwi, hii ni kwa sababu mnatuona nyani', 'imefika mahali kwenye hii nchi kila anayepinga dhuruma anaitwa mkaidi, anaharibu amani ya nchi, mara mchochezi, hii ni kwa sababu mnatuona nyani'.

Kamanda Kuzaga aliwataka wananchi kuepuka kufanya vitu ambavyo vinaashiria uvunjifu wa amani kwa maelezo kuwa watakumbana na mkono wa sheria.

# Serikali yapewa siri kupata wahandisi wengi wanawake

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya CPS inayotekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za kisasa eneo la Fumba Town, imesema watoto wa kike wanahitaji kujengewa uwezo wa kusoma masomo ya sayansi, ili Zanzibar iwe na wahandisi wengi wanawake.

Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Katrin Dietzold Nyamanzi, alitoa rai hiyo Wilaya ya Magharib B Unguja, katika hafla ya kuwapongeza wasichana waliomaliza fani ya uhandisi ambao wamewezeshwa na kampuni hiyo.

Alisema licha ya kampuni hiyo kuwa na programu ya ujenzi wa nyumba za kisasa lakini inaprogramu mbalimbali za kuisaidia jamii ikiwamo ya kuwasomesha wasichana katika fani ya uhandisi na baada ya kumaliza masomo huwaajiri katika kampuni hiyo.

Nyamanzi alisema hatua hiyo itasaidia kuinua kipato cha wanawake lakini pia kuhamasika kusoma fani ya uhandisi kwa sababu baada ya kumaliza masomo wanauhakika wa kupata ajira katika kampuni hiyo.

Alisema wasichana waliowafadhili masomo yao ya uhandisi wamehitimu katika vyuo mbalimbali ikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Saalam (UDSM) na kwa sasa wameshapata ajira katika kampuni ya CPS.

Mkuu wa Wilaya ya magharib B Unguja, Hamida Mussa Khamis, aliwataka wazazi na walezi kuwahamasisha watoto wa kike kusoma fani ya uhandisi na kuwapa nguvu ya kujiamini ili kuongeza wataalamu katika fani hiyo visiwani Zanzibar.

Alisema Zanzibar bado inaidadi ndogo ya wanawake waliosomea fani ya uhandisi kutokana na mitazamo hasi ya jamii kuwa masomo ya sayansi ni ya wanaume, hivyo ni vyema kuondokana na mitazamo hiyo.

"Mitazamo hiyo imesababisha watoto wa kike kushindwa kuonesha uwezo wao walionao katika kukabiliana na changamoto za ajira ama vipaji katika maeneo mbalimbali," alisema.

Pia aliwataka wanawake waliohitimu mafunzo hayo kuhakikisha wanayafanyia kazi na kuonesha uwezo wao na kuwa mabalozi wa kuwahamasisha wenzao kusoma fani hiyo kwa kuwashika mkono kama walivyoshikwa wao.

Aliipongeza kampuni ya CPS kwa kutoa mafunzo hayo ambayo yanasaidia kuibua vipaji vya wanawake wahandisi na kuongeza ujuzi katika fani hiyo na kupata nafasi ya kuajiriwa.

Naye Mkuu wa Idara ya Mihimili na Ujenzi kutoka UDSM, Dk. Fatma Mohammed, aliipongeza CPS kutoa mafunzo kwa wanafunzi hao na kuwapatia ajira hali ambayo itawasaidia kujikwamua kiuchumi.

Alisema UDSM asilimia 25 wanaosoma fani ya uhandisi ni wanawake na wengi wao wanaishia njiani kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo gharama.

Mmoja wa wanafunzi, Sultana Mohammed Nassor na Debora Banita ambao tayari wameshapata ajira katika kampuni ya CPS waliwataka wanawake wenzao kutokuwa waoga wa kusoma fani ya uhandisi bali wajiamini ili kutimiza ndoto zao.



Wanawake wa Vitongoji vya Luhondo, Mafisa na Losiai vilivyopo Kijiji cha Makelele, Kata ya Pagwi Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga, wakisomba mchanga kwa ajili ya ujenzi wa shule inayojengwa katika kitongoji cha Losiai ili kuwanusuru watoto wao kutembea umbali wa kilometa saba hadi kijiji mama cha Makelele. **PICHA: DEGE MASOLI**

## Nchi za Afrika zapewa ushauri uboreshaji miundombinu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NCHI za Afrika zimetakiwa kubadilishana rasilimali na uzoefu, ili kuifanya sekta ya miundombinu katika bara hilo kuwa endelevu na kukidhi mahitaji ya jamii.

Hayo yalisemwa na Kamishna wa Miundombinu na Nishati wa Umoja wa Afrika (AU), Dk. Amani Abou-Zeid wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu Afrika ya miaka 10 (PIDA) uliofanyika visiwani hapa.

Dk. Amani alisema ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa miundombinu katika nchi hizo unanafasi kubwa wa kuimarisha miundombinu.

Alisema kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa taarifa baina ya nchi na nchi, hivyo ni vyema kufanya kazi kwa pamoja na kuhakikisha taarifa zinapatikana na kila nchi inatekeleza miradi yake.

Naye Makamu Mkuu wa Rais wa Afrika Mashariki ya Kati kutoka Shirika la Uwakala wa Kimataifa la Japan (JICA), Ando Naoki alisema shirika hilo litaendelea kushirikiana na kuzisaidia nchi za Afrika katika mipango yake ya maendeleo kwa sababu ukanda huo ni eneo huru la biashara.

"Changamoto iliyopo ni muunganiko kati ya nchi moja na nyingine na ndiyo maana JICA tupo hapa kuunga mkono katika kuimarisha miundombindu," alisema.

Mkurugenzi wa Miundombinu, Biashara na Viwanda Mtangamano wa Kikanda AU, Amine Idriss, alisema nchi wanachama wanapaswa kuchangia katika uwajibikaji ili kuleta mabadiliko.

Alisema mradi wa PIDA umeonyesha jinsi ambavyo wanaweza kutekeleza miradi mingi ambayo inaleta matokeo chanya kwa nchi za Afrika na wananchi zaidi ya milioni 20 kupata nishati ya uhakika.

# Kampuni zaungana kuimarisha upatikanaji gesi Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Oryx Gas Zanzibar Limited imeungana na Kampuni ya TP Company Limited ya Zanzibar, ambayo ni kampuni tanzu ya Vigor Turky's Group of Companies, ili kuimarisha ugavi na usambazaji wa gesi ya LPG visiwani hapa.

Hatua hiyo inafuatia uundwaji wa kituo cha kwanza cha gesi ya LPG visiwani hapa, ikiwa ni sehemu ya dhamira ya Oryx Energies Group kutimiza ajenda ya mpito ya nishati, ambayo inahusisha kuhakikisha upatikanaji wa gesi hiyo kwa masoko ya Afrika na hasa kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, Meneja Mkuu wa Oryx Gas Zanzibar, Shuwekha Khamis, alisema mali hizo zitabadilishwa na kuwa chini ya jina la Oryx Energies na TP Company Limited itachukua asilimia 30 ya hisa za Oryx Gas Zanzibar Limited.

"Makubaliano haya yatakuwa na sifa za kipekee, yakiweka mwanga kwa dhamira ya Oryx Energies kama kampuni kusaidia mipango ya jamii na kukuza ushirikiano wa ndani," alisema.

Alisema kampuni hiyo ya uendeshaji wa kituo kipya cha LPG, Oryx Gas Zanzibar itawasambazia gesi wateja wengine na hivyo kusaidia upatikanaji wa gesi ya uhakika, endelevu na usio na vikwazo kwa wakazi wa Zanzibar.

Aidha, alisema hatua hiyo pia inashughulikia hali ngumu ya kihistoria ya usambazaji wa ndani wa gesi ya kupikia, ambapo taratibu nyingi za uendeshaji na usimamizi zimeongeza gharama kwa Wazanzibari na mara nyingi kusababisha vikwazo.

Shuwekha alisema, maendeleo hayo ya ushirikiano na kampuni kubwa ya ndani ya nchi yanahakikisha dhamira yao ya kuwapatia wakazi wa Zanzibar nishati safi ya kupikia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Vigor Group, Abdallah Salim Turky, alisema, kuundwa kwa kituo kipya cha LPG kunaendana kikamilifu na maono yao ya kuwa mstari wa mbele katika kutoa bidhaa na huduma za hali ya juu ndani ya nchi kutoka kwa masoko ya kimataifa kufikia jamii kwa bei nafuu.

Alisema: "Hii itasaidia kuboresha viwango vya afya na ustawi wa Zanzibar na pia itasaidia kulinda mazingira kwa kutoa njia mbadala, salama na ya uhakika kwa matumizi ya mkaa na kuni."

# Adaiwa kumuua hawara wa bintiye kwa sumu

**Na Moses Ng'wat, SONGWE**

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia Mitedi Mwambughi (63) kwa tuhuma za kumuua kijana anayedaiwa kuwa ni hawara wa binti yake kwa kumnywesa sumu inayodhaniwa kuwa ni ya kuulia panya.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kumnywesha sumu, Christopher Mwamengo (23), kwa kumweka kinyumba bintiye huyo (19), wakati akijisubiri kujiunga na chuo baada ya kumaliza kidato cha sita mwaka huu.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Rashid Ngonyani, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 13 mwaka huu katika Kijiji cha Ikonya, Kata ya Bara, Wilaya ya Mbozi.

Ngonyani alisema inadaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alichukua uamuzi wa kumywesha sumu kijana huyo kama njia ya kulipiza kisasi baada ya kumtorosha bintiye na kumweka kinyumba kwa zaidi ya siku mbili bila ridhaa yake.

"Mbinu aliyotumia mtuhumiwa kutekeleza mauaji hayo ni kumtumia binti yake kumwita marehemu nyumbani kwake kwa lengo la kumwuliza kwanini alimchukua binti bila ridhaa yake ndipo alipompatia sumu," alisema.

Ngonyani alisema baada ya kijana huyo kupatiwa sumu, alianza kujisikia vibaya na kukimbizwa hospitalini na kufariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

"Tumefanya uchunguzi wa awali kwa kushirikiana na madaktari wa Hospitali ya Wilaya ya Mbozi na sampuri zimepelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kubaini sumu ya aina gani ambayo alilishwa," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbozi, Dk. Kelvin Masea, alithibitishwa kupokewa kwa Christopher hospitalini huko Septemba 13 mwaka huu usiku na kufariki dunia wakati anapatiwa matibabu.

"Alipokelewa hapa akiwa mahututi, hajitambui na daktari wa zamu alimhudumia kwa saa mbili tu kabla hajapoteza uhai wake," Dk. Masea.

Alisema timu ya madaktari kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walifanya uchunguzi wa awali kwa kuchukua sampuli ambazo zimepelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi ili kubaini aina ya sumu aliyolishwa na kusababisha kifo chake.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga ( wa tatu kushoto), akiingia jana Kiwanda cha Mati Super Brands Limited kukagua uwekezaji akiwa na maofisa wa kiwanda hicho walioongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, David Mulokozi (wa nne kushoto) ambaye ni mwekezaji mzawa. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Bil. 1/- kufadhili wanafunzi vyuo vikuu

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 65 wanatarajiwa kupatiwa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ufadhili wa masomo kwa mwaka wa masomo 2023/24.

Hiyo ni baada ya Benki ya NMB kufungua rasmi dirisha la pili wa ufadhili wa masomo na usimamizi mwaka 2023/24 kwa wanafunzi wanaojiunga vyuo vikuu kupitia Programu ya NMB Nuru Yangu Scholarship and Mentorship.

Benki hiyo itafadhili wanachuo 65 kwa Sh. bilioni moja; gharama zinazojumuisha ufadhili wa wateule 65 wa dirisha la kwanza, hivyo kufanya idadi ya wanufaika kufika 130.

Ufadhili huo unatolewa kupitia NMB Foundation ambayo inajikita katika kusimamia na kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta za kilimo, elimu, afya, mazingira na ujasiriamali. Mwaka jana ilifadhili wanafunzi 65 wanaoendelea na masomo katika vyuo vikuu mbalimbali.

Katika ufunguzi huo unaoanza Septemba 15 hadi Oktoba 8 mwaka huu, Meneja Mkuu wa NMB Foundation, Nelson Karumuna, alitaja sifa za waombaji kuwa ni ufaulu wa kidato cha sita wa daraja la kwanza pointi tatu hadi daraja la kwanza pointi saba, kwa wanafunzi wenye mazingira magumu na wenye changamoto.

"Ufadhili huu ambao unakwenda katika maeneo ya ada, nauli, posho, steshenari, mafunzo kwa vitendo na kompyuta mpakato, unatolewa kwa wanafunzi wanaojiunga chuo katika fani za Hesabu na Takwimu, Biashara, Uchumi, Teknolojia, Habari na Mawasiliano, Uhasibu, Uhandisi, Mafuta na Gesi, Sayansi pamoja na Udaktari.

"Mwaka huu tutafadhili wanafunzi 65, hivyo kutufanya kuwa na wanafunzi 130 hadi mwaka wa masomo wa 2023/24 utakapoanza. Programu hii pia inatoa usimamizi maalum kuwawezesha wateule kupata ushauri, tukitarajia kuibua vipaji na kuwasaidia vijana hao kutimiza ndoto zao kielimu.

"Tunawahamasisha Watanzania wote kufikisha taarifa hizi kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita mwaka huu, ambao wanajiandaa kujiunga na vyuo vikuu, kutembelea tovuti yetu, wajaze fomu kwa usahihi ili kuepuka makosa yanayoweza kuwatoa katika mchakato," alisema Karumuna. Mwenyekiti wa Bodi ya NMB Foundation, Ruth Zaipuna, aliweka msisitizo kauli ya Meneja Mkuu wake, akiwataka waombaji wahakikishe wanajaza fomu zao kwa usahihi, ili kuepuka makosa kama yaliyochangia kutopata wanafunzi 100 waliowahitaji mwaka jana, badala yake wakapata 65 tu.

"Mwaka jana tulitoa nafasi 100, lakini hadi dirisha la usajili linafungwa, tulipata wanafunzi wenye sifa 65 tu, kutokana na wengi kufanya makosa katika ujazaji wa fomu, tukajikuta wapo wanafunzi wenye sifa wameondolewa kwenye mchakato wakati walikuwa wanastahili ufadhili wetu. Tunaomba makosa hayo yasijirudie.

"Nia yetu kubwa ni kuwa chachu ya maendeleo endelevu ya vijana wa Kitanzania na jamii kwa ujumla. Pamoja na ufadhili huu wa masomo tunaowapa, pia tutaendelea kuwatafutia wateule wetu nafasi za mafunzo kwa vitendo, sio tu hapa kwetu, bali pia kwa taasisi washirika watakaoungana nasi.

"Mwisho kabisa, niwahakikishie vijana watakaoomba na Watanzania kwa ujumla, kwamba mchakato huu utakuwa wa huru, wenye usawa, haki, uwazi na umakini, ili kupata vijana wanaostahili. Tutafanikisha mchakato huu kupitia matawi yetu 230 yaliyoko kote nchini na Mamlaka za Serikali za Mitaa," alisema Zaipuna.

## Mtoto afariki dunia akiogelea Ziwa Victoria

**Na Restuta Damian, KAGERA**

MTOTO anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 14, mkazi wa Wilaya ya Ngara mkoani hapa, amekufa maji na mwenzake kuokolewa baada ya kuzama wakati wakiogelea Ziwa Victoria.

Ofisa Habari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapa, Shambani Mussa, alisema mtoto huyo ambaye jina lake halijafamika, alikumbwa na mkasa huo Septemba 14 mwaka huu.

Mussa alisema mtoto huyo na mwenzake huyo, Mganyizi Longino (12) kutoka wilayani Ngara, wakiwa wageni katika mjini wa Bukoba, walikutana na kwenda kuogelea ziwani humo.

Alisema mwili wa mtoto huyo uliopolewa na kukabidhiwa kwa Jeshi la Polisi ili waupeleke kuuhifadhi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Kagera kusubiri ndugu kuuchukua kwa maziko.

"Ilikuwa siku ya kwanza Mganyizi kufahamiana na rafiki yake kwa kuwa awali walikutana eneo la stendi ya Bukoba na kupanga safari ya kwenda kuogelea," alisema.

Alisema wakiwa eneo la fukwe za ziwa hilo, walianza kuogolea ndipo mwenzake maji yalimzidi nguvu kumsogeza mbali, ambako alizama na kufa.

"Tulivyoingia kwenye maji wanaanza kuogelea yeye maji yakamzidi nguvu yakamsogeza mbali, lakini mimi vijana walikuja kuniokoa lakini yeye walishindwa kumtoa," alisema Longino.

## Wawili wafa mgodini wakichimba dhahabu

**Na Said Sindo, GEITA**

WATU wawili wamefariki dunia wakati wakichimba madini katika mgodi uliofungwa wa Kanegere wilayani Mbogwe baada ya kuangukiwa na kifusi cha mchanga.

Waliofariki dunia ni Justine Godwin (23), mkazi wa Katoro na Wilson Masunga (23), mkazi wa Bariadi mkoani Simiyu.

Manusura Musa Maduhu na Innocent Mihayo walisema kuwa waliingia ndani ya shimo hilo saa tano usiku na kuwakuta wenzao zaidi ya 20 wakichimba na walipoomba wachimbe walikataliwa, hivyo wakatoka ndani ya shimo hilo.

Walisema kuwa baada ya muda waliporejea shimoni humo walikuta wenzao wamedondokewa na kifusi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Safia Jongo, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 10 mwaka huu katika mgodi huo ambapo watu 30 walifukiwa na kifusi na kati yao, 28 waliokolewa wakiwa hai.

Kamanda Jongo alisema wachimbaji hao, maarufu Manyani, walivamia katika mgodi huo ambao ulikuwa umefungwa kufanya shughuli za uchimbaji.

Alisema watu hao waliingia mgodini humo kwa njia zisizo rasmi na kuanza shughuli ya uchimbaji.

HABARIKIMATAIFA

# Vifo mafuriko vyafikia 11,300

**Derna, LIBYA**

MAFURIKO yaliyotokea wiki iliyopita Libya pamoja na kimbunga Daniel yameua watu 11,300 katika mji wa Derna, kulingana na ripoti mpya iliyochapishwa mwishoni mwa wiki, Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) limesema.

"Kulingana na Shirika la Hilali Nyekundu la Libya, mafuriko haya ambayo hayajawahi kutokea yalisababisha vifo vya watu 11,300 na wengine 10,100 kutoweka katika mji wa Derna pekee," ilitangaza Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA).

Takriban watu 170 pia walifariki dunia katika maeneo mengine mashariki mwa Libya, Ocha iliongeza, "Idadi hii inatarajiwa kuongezeka wakati timu za utafutaji na uokoaji zikifanya kazi usiku na mchana," UN ilionya.

Kimbunga Daniel kilipiga mji wa Derna, wenye wakazi 100,000, usiku wa Jumapili wiki iliyopita, kuamkia Jumatatu Septemba 11. Hali hiyo ilisababisha kupasuka kwa mabwawa mawili ya maji ya mto na kusababisha mafuriko ya ukubwa wa tsunami.

Maji hayo yalisomba kila kitu na kusababisha vifo vya maelfu ya watu. Makumi ya miili hutolewa nje na kuzikwa kila siku.

Waziri wa Afya wa Utawala wa Mashariki mwa Libya, alitangaza idadi ya vifo vya watu 3,252 Jumamosi jioni. Shirika la Afya Duniani (WHO), lilisema hapo awali kwamba miili ya watu 3,958 ilipatikana na kutambuliwa.

"Zaidi ya watu 9,000 bado hawajapatikana." Kulingana na shuhuda za wakazi wengi wa waathiriwa walikwama chini ya matope au kusombwa hadi katika Bahari ya Mediteranian.

Aidha, Russia, imesema imepeleka madaktari wa dharura 35 pamoja na misaada katika eneo la mashariki mwa Libya, baada ya taifa hilo kukumbwa na mafuriko makubwa wiki iliyopita.

Taarifa ya Wizara ya Masuala ya Dharura ya Russia, ilisema kwamba ndege ya tatu iliyokuwa na madaktari wabobezi imekwishatua Libya, ikiwa na karibu watumishi 35 wa wizara, watatoa huduma za afya kwa waathirika.

Tayari imepeleka hospitali za kuhamishika, zenye vyumba vya upasuaji na huduma za uangalizi maalumu.

Aidha madaktari hao 35 watatoa huduma maalumu za tiba kwa hadi watu 100 kwa siku kwenye maeneo waliko waathiriwa, ilisema wizara hiyo.

**DW/RFI**



Mkazi akiwa amekaa mbele ya nyumba yake katika eneo la Derna, lililoathirika vibaya na mafuriko nchini Libya, mwishoni mwa wiki. **PICHA: DW**

# Ajali ya ndege yaua 14 Brazil

**Amazon, BRAZIL**

WATU 14 wamefariki dunia katika ajali ya ndege kufuatia hali mbaya ya hewa katika eneo la Amazon nchini hapa mwishoni mwa wiki.

Ndege hiyo ndogo ya propela, ilikuwa inakaribia mwisho wa safari yake ya kilomita 400 (maili 248) kati ya Manaus, mji mkuu wa jimbo la Amazonas na mji wa mbali wa msitu wa Barcelos ilikoanguka.

Maofisa walisema wote waliokuwa ndani ya ndege hiyo, abiria 12 na wafanyakazi wawili, walifariki dunia katika ajali hiyo. Uchunguzi umeanzishwa kubaini chanzo cha tukio hilo.

Waziri wa Usalama wa Jimbo la Amazonas, Vinicius Almeida, alisema taarifa za awali zilidokeza kwamba ndege hiyo ilianguka baada ya kupoteza mwelekeo, wakati ilipokuwa ikitua Barcelos.

**BBC**

**Maofisa walisema wote waliokuwa ndani ya ndege hiyo, abiria 12 na wafanyakazi wawili, walifariki dunia katika ajali hiyo. Uchunguzi umeanzishwa kubaini chanzo cha tukio hilo.**

# Waziri Mkuu aagiza uuzwaji mafuta kwa bei ya hasara

**Paris, UFARANSA**

WAZIRI Mkuu wa Ufaransa, Élisabeth Borne, ametangaza hatua mpya ya kukabiliana na mfumuko wa bei ya mafuta, huku bei zikitishia kuvuka euro mbili kwa lita.

"Wadau wa biashara ya mafuta wataruhusiwa kuuza petroli kwa hasara kwa miezi michache."

Borne, ametangaza kwamba waagizaji na wasambazaji wa mafuta wataweza kuuza petroli kwa hasara kwa miezi michache, ili kuwaruhusu kupunguza bei zaidi katika mahojiano yaliyotumwa mtandaoni, mwishoni mwa wiki.

"Kwa hatua hii ambayo haijawahi kushuhudiwa, tutakuwa na matokeo yanayoonekana kwa Wafaransa, bila kutoa ruzuku ya mafuta," alisema, baada ya kukumbusha kuwa kuuza kwa hasara kumepigwa marufuku na sheria tangu 1963.

Mkuu wa serikali hiyo, hakukubali mapendekezo ya upinzani ambayo yanataka aidha punguzo kama mwaka mmoja uliopita au kupunguzwa kwa ushuru wa petroli, ili kukabiliana na kupanda kwa bei ya mafuta ambayo imefikia euro mbili kwa lita.

"Kila mtu anachukua sehemu yake, ni kawaida kuwashirikisha wanaviwanda wakubwa," huku akikumbusha kuwa jukumu la serikali pia ni kupunguza nakisi yake na deni lake.

Vyama vya vituo vya mafuta vinachukulia hatua hiyo kuwa haiwezekani. Tangazo hilo, limemshangaza Francis Pousse, kiongozi wa chama cha vituo vya mafuta cha Mobilians ambacho kina vituo vya mafuta 5,800 vya huduma za kitamaduni, bila kujumuisha maduka makubwa.

Alisema hatua hiyo mpya ni jibu kwa maduka makubwa, kuwaruhusu kupambana katika sekta, hiyo yenye ushindani mkubwa, wakati bei ya mafuta kwenye masoko ya kimataifa hivi karibuni itazidi euro 1.99.

"Sisi, wauza mafuta, hakuna suala la kuuza kwa hasara," ameliambia shirika la habari la AFP. Kabla ya kuongeza: "Wanachama wangu wanaishi kwa 40, asilimia 50 au hata zaidi kutokana na uuzaji wa mafuta, kwa hivyo ikiwa watauza kwa hasara, ninawapa miezi mitatu." Akinukuliwa Waziri Mkuu.

Katika soko ambalo tayari limebanwa sana, anaonyesha kwamba kiwango cha jumla cha vituo vya jadi ni senti moja hadi mbili kwa lita katika nyakati za kawaida.

Pousse pia anasema ana shaka kuhusu athari za hatua hiyo, kwa wanunuzi. Kwa sababu ikiwa bei za wauzaji wa maduka makubwa zitaendelea kuongezeka, hawataweza kumudu kupoteza senti 15 kwa kila lita ya petroli".

Hakuna msambazaji au mwagizaji wa mafuta aliyetoa maoni yake kufuatia tangazo la mkuu wa serikali.

**RFI**

# POLISI TANZANIA, PAMBA ZATAKATA CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Pamba FC ikipata ushindi wake wa pili mfululizo juzi katika Ligi ya Championship, Polisi Tanzania iliyoshuka daraja msimu uliopita, imepata ushindi wake wa kwanza.

Jamal Mtegela alifunga bao pekee kwa mkwaju wa penalti dakika ya 73 na kuifanya Pamba yenye maskani yake Mwanza kupata ushindi wa pili mfululizo kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Katika mechi ya ufunguzi iliishindilia Cosmopolitan ya Dar es Salaam mabao 4-0.

Kwa matokeo hayo ya juzi, Pamba inaongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa kwenye raundi ya pili kwa pointi sita na mabao matano.


Polisi Tanzania ambayo msimu uliopita ilicheza Ligi Kuu na kuteremka daraja, ilipata ushindi wa kwanza kwenye Championship, ikiifunga Ruvu Shooting ambayo iliteremka nayo daraja bao 1-0.

Alikuwa ni Denis Mushi aliyeukwamisha mpira wavuni na kuwa bao pekee kwenye mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, Kilimanjaro.

Katika mechi ya kwanza, Polisi Tanzania ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya Kwanza na baada ya mechi hiyo sasa inapanda hadi nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo.

Matokeo mengine ya ligi hiyo, TMA ikaidungua Biashara United bao 1-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, KenGold ikipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Green Warriors, mechi ikichezwa, Sokoine Mbeya, na Copco ikaishindilia Cosmopolitan mabao 3-1 katika Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, ikiwa ni kipigo cha pili mfululizo kwa Cosmo inayoshika mkia ikiwa haina pointi na kuruhusu jumla ya mabao saba hadi sasa.

**PENYA...**




Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akijaribu kuipenya ngome ya Al-Merrikh kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Kigali Pele nchini Rwanda Juzi na Yanga kushinda mabao 2-0. **PICHA: YANGA**

# Kipanga kufuta makosa ikiivaa Jamhuri leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kipanga imesema itaendelea kukiimarisha kikosi chake ili kufanya vizuri katika mchezo ujao na kuibuka na alama zote tatu.

Kipanga FC katika mchezo wao wa kwanza ililazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Malindi SC katika mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), mchezo uliochezwa Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na Nipashe, Kocha wa Maafande hao wa Kipanga, Hassan Abdulrahman, alisema kuelekea mchezo wao wa pili ambao watashuka dimbani dhidi ya Jamhuri leo, atasawazisha makosa yote ambayo ameyaona katika mchezo wao kwanza hasa suala la umakini.

Alisema timu yake katika kipindi cha pili wamepoteza nafasi nyingi za wazi kutokana na washambuliaji kutokuwa makini hasa wanapokuwa katika lango la wapinzani wao.

Kocha huyo alisema licha ya kucheza na timu ngumu ya Malindi, lakini wangekuwa na uwezo wa kupata alama tatu iwapo wachezaji wao wangetulia katika nafasi zao.

"Wachezaji walicheza vizuri japo makosa madogo yaliyojitokeza ambayo yalisababisha mpaka kupata sare, bado wachezaji hawajatulia katika nafasi zao, kupoteza umakini pale tunaposhambulia, hivyo makosa haya yatafanyiwa kazi katika mchezo ujao," alisema.

Aidha, mchezo uliochezwa Kisiwani Pemba katika Dimba la FInya, wenyeji timu ya Maendeleo walijikuta wakipokea kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Maafande wa KVZ.

## ZFF yaanza hamasa mashabiki viwanjani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Suleiman Salum, amesema jitihada kubwa zinahitaji ili kurejesha hamasa kwa mashabiki wa soka visiwani Zanzibar kuweza kuifuatilia Ligi Kuu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema jitihada hizo si tu kuwaachia kamati ya hamasa au vyombo vya habari pekee, bali Wazanzibari wote kwa ujumla wanayo nafasi ya kuhamasishana kwenda viwanjani kushuhudia michezo ya Ligi Kuu.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa juma, mwenyekiti huyo alisema yeye binafsi ni mdau mkubwa wa soka la Zanzibar, hivyo anatamani kuona mashabiki wanajitokeza kwa wingi kushuhudia mechi mbalimbali za ligi hiyo.

Alisema katika kuhakikisha hilo linafanikiwa kwa kushirikiana na Kamati ya Hamasa ya ZFF, ameanza ziara katika mitaa mbalimbali ya Unguja kwa kukutana na wadau wa soka ili kuwahamasisha kufuatilia ligi yao kwa kwenda viwanjani.

"Tunataka kurejesha hamasa ya mpira hapa nyumbani, hivyo hatuwezi kurejesha hamasa kama hatutakuwa na njia ya kuwarejesha hao mashabiki tunaowataka, ndio maana tumeanza huu mpango wa kupita katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu ili kuhamasisha jamii kuja uwanjani na kufatiliwa Ligi ya Zanzibar kama wanavyofanya kwenye ligi nyingine," alisema.

## Ngumi za Ufukweni kupigwa Oktoba

**Na Shufaa Lyimo**

MAPAMBANO ya mchezo wa Ngumi za Ufukweni (Safari ya Beach), yanatarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, kwenye fukwe za Msasani jijini Dar es Salaam, imethibitishwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa mapambano hayo, Promota Meja Selemani Semunyu, alisema kutakuwa na mapambano mengi ya mabondia chipukizi na kwamba muda wowote kuanzia sasa atatangaza pambano moja la bondia kutoka nje ya nchi.

"Nimeamua kuwapa nafasi vijana nikiwa na lengo la kutengeneza vipaji vipya ambavyo miaka ijayo vitapeperusha bendera ya Tanzania kupitia mchezo huu," alisema Meja Semunyu.

Alisema ameamua kuwapa nafasi vijana kutokana na kugundua vipaji vingi na kuwataka wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi siku ya mapambano hayo ili kushirikiana naye.

Aliongeza kuwa, pia kutakuwa na mapambano ya wanawake likiwamo lile la Zawadi Kutaka atakayepambana na bondia kutoka nchini Kenya ambaye atamtangaza baadaye.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SANCHO ATAKIWA BARCA

BARCELONA wana nia ya kutaka kumnunua winga wa Manchester United na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, licha ya masaibu yanayomkumba Old Trafford. **(Sport)**

### ARSENAL KUMUUZA PARTEY

KIUNGO wa Arsenal na Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 30, huenda akauzwa Januari huku Juventus ikitarajiwa kuwa kituo chake. **(Football Insider)**

### WILDER AWINDWA SHEFFIELD

KLABU ya Sheffield United inapania kumchukua kocha wao wa zamani, Chris Wilder kama mbadala wa Paul Heckingbottom. **(Mail)**

### ODEGAARD MKATABA MPYA

ARSENAL Inakaribia kuafiki mkataba mpya wa miaka minne na kiungo wa kati wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 24, ambapo atalipwa pauni 200,000 kwa wiki. **(Football Insider)**

### RONALDO AISHTAKI JUVENTUS

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 38, anaishtaki klabu yake ya zamani ya Juventus katika harakati ya kutafuta pauni milioni 17 kama mshahara ambao hakulipwa wakati wa janga la Covid-19. **(Gazzetta dello Sport)**

### DE JONG, BARCA BADO

BARCELONA bado hawajajadili mpango wa kuongeza mkataba wa mchezaji Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 26, huku mkataba wa sasa wa kiungo huyo wa Uholanzi ukitarajiwa kumalizika mwaka 2026. **(Marca)**

### GNONTO ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton bado ina nia ya kumsajili winga wa Leeds na Italia, Wilfried Gnonto mwenye umri wa miaka 19, baada ya kushindwa katika msimu wa majira ya joto. **(Football Insider)**

### ALONSO AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich iko mbioni kumwajiri kiungo wa kati wa zamani wa Hispania na kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso kama kocha kuelekea msimu ujao. **(Mundo Deportivo)**

### GALLAGHER ARIDHIKA CHELSEA

CONOR Gallagher kwa sasa ameridhika kuwa Chelsea, ingawa Tottenham Hotspur inapanga kurejelea tena azima ya kumnunua katika dirisha la Januari, kiungo huyo wa England mwenye umri wa miaka 23. **(Football Insider)**


### WILLIAMS ANYATIWA BARCA

KLABU ya Athletic Bilbao ina imani Nico Williams atasaini mkataba mpya, licha ya Barcelona kuonesha nia ya kumsajili winga huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 21, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao. **(Sport)**

### EVERTON HAIPO SOKONI

MPANGO wa 777 Partners wa kuinunua klabu ya soka ya Everton uko mashakani baada ya uchunguzi kuanzishwa kutokana na hoja iliyoibuka kuhusu uwekezaji wa kampuni hiyo katika mpira wa kikapu wa England. **(Telegraph)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FELIX: NAFURAHIA MAISHA MAPYA HAPA BARCELONA

●●●Unapokuwa na muundo mzuri na kuzunguka mpira kwa kasi, nafasi zinaonekana na pia...

**BARCELONA, Hispania**

JOAO Félix amesema anafurahia maisha ndani ya Barcelona baada ya kufunga bao lake la kwanza katika ushindi wa mabao 5-0 Jumamosi dhidi ya Real Betis kwenye Ligi Kuu Hispania, La Laiga.

Félix, ambaye alijiunga na Barca kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Atletico Madrid mwezi huu, alifunga bao la kwanza kwenye Uwanja wa Olympic na kisha alitumia vizuri pasi ya Andreas Christensen na kusaidia kutengeneza bao la Robert Lewandowski.

Ferran Torres, Raphinha na João Cancelo pia walifunga wakati Barca ikipaa kileleni mwa LaLiga kwa muda kabla ya mchezo wa Real Madrid dhidi ya Real Sociedad jana Jumapili.

"Nina furaha sana kuanza kikosi cha kwanza, hisia ni nzuri sana ni rahisi kucheza katika timu hii," alisema Félix, ambaye alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo kule Chelsea.

"Unapokuwa na muundo mzuri na kuzunguka mpira kwa kasi, nafasi zinaonekana na pia mabao. Nina furaha, mabadiliko yamenifanya vizuri, mimi na familia yangu, nina furaha sana hapa."

Félix mwenye umri wa miaka 23, ameungwa mkono na kustawi Barca baada ya misimu minne ya kupanda na kushuka kule Atletico kutokana na uhamisho wake wa Euro milioni 126 kutoka Benfica ya Ureno mwaka 2019.

Vyombo vya habari vya ndani vimependekeza mtindo wa Barca utamfaa zaidi, ingawa kocha Xavi Hernandez hakutaka kuhusishwa na kulinganisha na Atletico, akisema "namheshimu sana" kocha wao, Diego Simeone.

Hata hivyo, Xavi aliwamwagia sifa wachezaji wawili waliosajiliwa hivi karibuni na Barca, huku Cancelo, ambaye amejiunga kwa mkopo kutoka Manchester City, pia akivutia mechi yake ya kwanza dhidi ya Betis.

"Joaos wote wana furaha hapa na unaweza kuona hilo," Xavi alisema katika mkutano na wanahabari.

"Hakuna anayetilia shaka ubora wao binafsi. Unawaona wakifanya mazoezi na unaona jinsi walivyo wazuri.

"Cancelo anajiunga nasi baada ya kufanya kazi na kocha bora zaidi duniani (Pep Guardiola) na anautafsiri mchezo vizuri sana. Anaelewa tunachotaka.

"Wote Cancelo na Félix wanatoa chaguzi zinazosaidia kuboresha timu. Kimwili, wako imara. Wanaongeza ubora kwenye kikosi. Wako pale wanapotaka kuwa."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
NOTTINGHAM
VERSUS
BURNLEY
1 | 2.26
X | 3.46
2 | 3.15

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: MAC ALLISTER ALICHOKA



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amefichua kwamba Alexis Mac Allister alijisikia “nafuu” kwa kutolewa nje baada ya Liverpool kufanya vibaya kipindi cha kwanza katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Wolves Jumamosi.

‘Wekundu hao walikuwa bila Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold, wakati Hwang Hee-chan alipofunga baada ya kazi kubwa kutoka kwa Pedro Neto na walikuwa na wakati mgumu wa kutengeneza nafasi katika kipindi cha kwanza.

Allister alikuwa na dakika 45 za kwanza baada ya kusafiri hadi Amerika Kusini kuichezea Argentina wakati wa mapumziko ya kimataifa, alipewa kadi ya njano mapema.

Kiungo huyo wa zamani wa Brighton, nafasi yake ilichukuliwa na Luis Diaz na Liverpool walisawazisha dakika ya 55 kupitia kwa Cody Gakpo kabla ya Andy Robertson kumalizia kwa akili na bao la kujifunga la Hugo Bueno kumpa Klopp ushindi wa mabao 3-1.

Klopp alikiri baada ya mabadiliko ya mchezo kuhitajika wakati wa mapumziko ili kuwarudisha Liverpool mchezoni, badala ya Mac Allister kuwa mmoja wao baada ya ratiba ngumu iliyojaa safari.

Alisema: “Jambo zuri katika kipindi cha kwanza ni kwamba ilikuwa mbaya kiasi kwamba sikufikiria kwamba tunaweza kucheza kipindi cha pili namna hiyo.

“Ni wazi tulitaka kuanza tofauti kabisa, lakini kwa sababu yoyote haikuwezekana.

“Kiwango kilikuwa chini. Hatukuweza kubadilika mara tano wakati wa mapumziko, kwa hiyo tulidhani tungebadilisha mfumo.

“Alikuwa na wakati mzuri katika kipindi cha kwanza, lakini hakukatishwa tamaa kuondoka, alipata nafuu zaidi.”

Wachezaji wengine wa akiba Darwin Nunez na Harvey Elliott walisaidia Liverpool kushikilia zaidi mechi hiyo baada ya kipindi cha kwanza.

# Ten Hag ajitetea kwa kuzomewa

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amepuuzia kuzomewa na mashabiki kwa uamuzi wake wa kumtoa Rasmus Højlund wakati wa kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Brighton, Jumamosi.

Siku mbaya kwa Ten Hag ilifanywa kuwa mbaya zaidi wakati uamuzi wake wa kumtoa Højlund na kumwingiza Anthony Martial katika kipindi cha pili ulichochea sauti kubwa kutoka kwa mashabiki.

“Nadhani ilikuwa nzuri,” alisema Ten Hag.

“Unaona mashabiki katika dakika ya kwanza pale Old Trafford, mapokezi ya (Højlund) yalikuwa mazuri. Nadhani alifanya vizuri sana. Ni vema wakatoa ishara hii, ujumbe huu. Itampa Rasmus imani.”

Højlund mwenye umri wa miaka 20 nusura aweke mechi yake ya kwanza United kwa kufunga bao, lakini akapata bao la kusawazisha kipindi cha kwanza lililokataliwa na VAR.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 72 majira ya joto alilazimika kusubiri kucheza mechi yake ya kwanza baada ya kuwasili kutoka Atalanta akiwa na jeraha la mgongo na Ten Hag alisema hakuwa na uwezo wa kucheza dakika zote 90 dhidi ya Brighton.

“Kila mtu anajua alikuja na suala dogo,” aliongeza.

“Tulimjenga kwa muda wa wiki tatu au nne zilizopita, lakini hayuko tayari kwa mchezo mzima na tuna michezo mingi ya kucheza kwa muda mfupi, kwa hivyo lazima tujitengenezee.

“Iwapo atajeruhiwa kwa sababu hana uwezo wa kucheza dakika 90 basi tuko mbali sana kuliko tunakotaka kuwa.”



CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# CHAMA ATAKA COASTAL KUWA DARAJA LA KUIMALIZA DYNAMOS

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba, Clatous Chama, anaamini mchezo unaofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union utakuwa sehemu ya kusahihisha makosa yao kuelekea mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, Oktoba Mosi, mwaka huu.

Chama ndiye aliyeisawazishia Simba mabao yote mawili katika sare ya 2-2, ikitokea nyuma dhidi ya Power Dynamos juzi katika Uwanja wa Levy Mwanawasa nchini Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Chama alisema kabla ya kuwaza mechi ya marudiano hapo kati kuna mchezo wa ligi, watakaporejea wataanza maandalizi ya mechi hiyo ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union kabla ya kurudiana na Power Dynamos.

"Hapa kati kuna mechi ya ligi, akili na nguvu tunaelekeza kwenye mchezo huo, tukimaliza mechi hiyo tunaingia katika maandalizi ya kupambana kwa ajili ya kusaka ushindi na kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ninaimani Dar es Salaam tutapambana zaidi, katika mpira chochote kinaweza kutokea sare ilikuwa si lengo letu, tunaenda kupambana katika mechi ya marudiano, " alisema Chama. Aliongeza kuwa mechi ilikuwa ngumu na wachezaji walipambana kuhakikisha wanasawazisha lakini Power Dynamos walibadilika tofauti na walivyocheza awali kwenye mechi ya Tamasha la Simba Day, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Chama alisema baada ya kufungwa bao la kwanza walifanikiwa kujiandaa kiakili na kimwili kwa kupeana ishara ya kupambana hadi hatua ya mwisho kusawazisha mabao.

"Muhimu sana kucheza kwa mahitaji ya timu, kocha na kuwapa furaha mashabiki wetu ambao wamekuwa pamoja na sisi katika kila hatua, hatuwezi kuwaambia kwa maneno bali kuhakikisha tunawafurahisha kwa matokeo mazuri uwanjani," alisema Chama.

# Simba, Yanga SC CAF haijaisha

INATOKA UK. 24

Akizungumza juzi baada ya dakika 90 kukamilika, Robertinho alisema wamepoteza nafasi tano za wazi za kufunga katika sare ya 2-2 dhidi ya Power Dynamos ambazo zingewawezesha kupata ushindi mnono ugenini.

Alisema kipindi cha kwanza hawakucheza vizuri na kuwapa nafasi Power

Dynamos kumiliki mpira lakini kipindi cha pili alifanya mabadiliko ambayo yalimsaidia kucheza vizuri na kutengeneza nafasi nyingi ambazo hawakuzitumia.

"Nawapongeza wachezaji kwa kazi kubwa waliyofanya katika mchezo huu, licha ya kupata sare, tumecheza vizuri hasa kipindi cha pili, tumetengeneza nafasi nyingi. Tumepoteza nafasi zaidi ya tano za kufunga lakini huu ndio mpira wa miguu tunarudi nyumbani kujipanga," alisema Robertinho.

Aliongeza kuwa sare waliyoipata ugenini ni matokeo mazuri, kwani itawasaidia, hivyo wanarudi katika uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yao ikiwamo safu ya ulinzi kulingana na mabao waliyofungwa na ushambuliaji kuwa makini na nafasi wanazotengeneza kuzitumia ipasavyo katika mechi ya marudiano ili kufuzu kucheza makundi.

Beki wa kati wa Simba, Che Fondoh Malone, alisema hawajakata tamaa, wanajipanga kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya Power Dynamos ili kufuzu hatua ya makundi.

Alisema bado wana nafasi ya kufanya vizuri katika mchezo wa marudiano na wamerudi kujipanga, kwani haukuwa mchezo rahisi na kwamba benchi la ufundi limeona makosa na anaamini watayafanyia kazi kwa ajili ya mechi ijayo.

"Hatujakata tamaa ya kusonga hatua ya makundi, tuna dakika 90 nyingine nyumbani ambazo tunaamini tutazitumia vizuri na kuingia hatua ya makundi," alisema Che Malone.

Kwa upande wa Yanga, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kutokana na uwezo mkubwa waliouonesha kwenye mechi hiyo ana uhakika wanaweza kuvunja rekodi ya kuwa timu ya kwanza Tanzania kucheza hatua ya nusu fainali au fainali ya michuano hiyo licha ya kwamba wamekuwa na muda mrefu hawajatinga katika hatua ya makundi.

Simba ndiyo timu yenye rekodi ya kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa misimu mitatu tofauti.

"Umeiona mechi ilikuwa nzuri na tunahitaji kupata matokeo mazuri, Al Merrikh si timu mbaya, ila ilibidi tucheze kwenye ubora wetu tunao wachezaji wenye uzoefu, wajanja, watulivu wa kucheza soka popote pale tukapata ushindi na kama tukiendelea hivi na tukiingia kwenye hatua ya makundi, sisi tunaweza tukawa ndiyo timu ya kwanza kuweka rekodi ya kwanza ya nchi ya kucheza hatua za mbele zaidi kuliko zilizowekwa hapo mwanzo," alisema Kamwe.

Al Merrikh iliutumia uwanja huo nchini Rwanda kutokana na nchini kwao, Sudan kuwa na machafuko ya kisiasa.

"Lilikuwa ni deni kubwa, ilibidi tuzungumze na wachezaji, tuwaeleze na tuwahimize kwamba tunahitaji kupata matokeo mazuri leo (juzi) kwa ajili ya mashabiki na wao walitusikiliza na hata wenyewe waliona jinsi majukwaa walivyojaa na kushangilia, kusema kweli wamewatendea haki mashabiki wetu, wamefurahi sana," alisema.

Alitamba kuwa kama wakifanikiwa kutinga hatua ya makundi na wakipangiwa na klabu za Afrika Mashariki basi watakuwa wakienda na kundi kama hilo au zaidi la mashabiki kiasi cha wao kuonekana wapo nyumbani badala ya wenyeji wao.

Hata hivyo, aliwakumbusha wanachama na mashabiki kuwa timu yao bado haijafanikiwa kutinga hatua ya makundi kwa muda wa miaka 24, hivyo wajiandae na mechi ya marudiano itakayochezwa Septemba 30 katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

"Kama kuna mwanachama na shabiki wa Yanga ajue kuwa klabu yake haijacheza Ligi ya Mabingwa Afrika kwa muda mrefu kwa hiyo ilikuwa ni lengo letu namba moja msimu huu ni kuingia hatua hiyo, ya Rwanda yamemalizika, sasa wakusanyike kama walivyofanya Kigali jijini Dar es Salaam na lengo litakuwa moja tu nalo ni kufuzu hatua ya makundi," alisema.

Mabao ya Yanga yalifungwa na Kennedy Musonda na Clement Mzize yaliyowaweka hatua moja kwenda makundi kwa mara ya kwanza tangu 1998. Kwa upande ya yale ya Simba yote mawili yalifungwa na Clatous Chama.

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 18/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3924 | Crewe U21 vs Hull City U21 | 3.52 | 4.29 | 1.72 |
| 16:00 | 2495 | FK Tyumen vs Rodina Moscow | 3.14 | 3.19 | 2.09 |
| 17:00 | 2568 | FK Jedinstvo UB vs FK Smederevo | 1.88 | 3.14 | 3.85 |
| 17:00 | 5796 | Dynamo Kiev vs Vorskla Poltava | 1.37 | 4.43 | 6.45 |
| 17:30 | 3885 | Roma Youth vs Frosinone Youth | 1.57 | 4.18 | 4.48 |
| 18:00 | 3139 | Atromitos vs Volos | 1.86 | 3.44 | 4.07 |
| 18:00 | 3362 | Floro vs Sogndal 2 | 2.07 | 3.84 | 2.73 |
| 18:00 | 5589 | Jazeera Amman vs Sama | 1.49 | 3.90 | 5.20 |
| 18:30 | 3963 | FC Politehnica Iasi vs Botosani | 2.20 | 3.07 | 3.22 |
| 18:30 | 4144 | FC Dynamo-Makhachkala vs FC Alania Vladikavkaz | 2.79 | 2.89 | 2.47 |
| 19:00 | 1093 | Maccabi Jaffa vs Ihud Bnei Shfaram | 2.04 | 3.37 | 3.42 |
| 19:00 | 1345 | Nea Salamis vs Ethnikos Achnas | 2.22 | 3.37 | 3.01 |
| 19:00 | 2139 | Gornik Leczna vs Resovia Rzeszow | 2.00 | 3.27 | 3.27 |
| 19:00 | 4222 | Nazareth Ilit vs Hapoel Kfar Saba | 1.99 | 3.63 | 3.32 |
| 19:00 | 4510 | Hapoel Afula vs SC Kfar Qasem | 2.33 | 3.26 | 2.90 |
| 19:00 | 4866 | HNK Sibenik vs Cibalia Vinkovci | 1.61 | 3.49 | 4.96 |
| 19:00 | 5703 | Talaea El Gaish vs National Bank | 2.68 | 2.45 | 3.28 |
| 19:15 | 1363 | Nancy vs Dijon | 2.55 | 3.40 | 2.50 |
| 19:30 | 4267 | Salernitana vs Torino | 3.46 | 3.20 | 2.23 |
| 20:00 | 1035 | Osters IF vs Vasteras SK | 2.02 | 3.62 | 3.36 |
| 20:00 | 1157 | Sakaryaspor vs Bodrumspor | 2.77 | 3.07 | 2.36 |
| 20:00 | 1174 | Jonkopings Sodra vs Landskrona Bois | 2.47 | 3.45 | 2.66 |
| 20:00 | 1212 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Hadera | 1.66 | 3.68 | 4.23 |
| 20:00 | 1766 | Sivasspor vs Ankaragucu | 2.32 | 3.25 | 2.89 |
| 20:00 | 2650 | Stal Mielec vs Zaglebie Lubin | 2.82 | 3.33 | 2.20 |
| 20:00 | 2721 | Odense vs Silkeborg | 2.71 | 3.76 | 2.28 |
| 20:00 | 3711 | Norrkoping vs Mjallby | 1.97 | 3.34 | 3.29 |
| 20:00 | 4253 | Fatih Karagumruk vs Hatayspor | 1.94 | 3.41 | 3.62 |
| 20:10 | 3371 | AIK Football vs Degerfors | 1.42 | 4.34 | 5.65 |
| 20:30 | 1622 | Hapoel Beer Sheva vs Hapoel Tel Aviv | 1.57 | 3.68 | 4.94 |
| 21:00 | 2849 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Ajax | 1.76 | 3.99 | 3.63 |
| 21:00 | 3163 | Emmen vs Jong Utrecht | 1.36 | 4.71 | 6.76 |
| 21:00 | 3574 | FC Eindhoven vs ADO Den Haag | 2.19 | 3.47 | 2.86 |
| 21:00 | 4250 | De Graafschap vs Helmond Sport | 1.65 | 3.84 | 4.40 |
| 21:00 | 5626 | Univ San Martin vs Deportivo Coopsol | 1.74 | 3.28 | 4.34 |
| 21:00 | 5800 | Groningen vs Jong PSV | 1.47 | 4.29 | 5.51 |
| 21:00 | 5817 | FC Oss vs Dordrecht | 2.07 | 3.43 | 3.12 |
| 21:30 | 2601 | Sampdoria vs Cittadella | 2.27 | 3.08 | 3.08 |
| 21:30 | 2606 | CFR Cluj vs Petrolul Ploiesti | 1.44 | 4.06 | 6.78 |
| 21:45 | 2356 | Nuova Monterosi vs Latina | 2.92 | 3.29 | 2.36 |
| 21:45 | 2556 | Verona vs Bologna | 3.08 | 3.29 | 2.37 |
| 21:45 | 2870 | Guingamp vs AC Ajaccio | 2.20 | 3.12 | 3.17 |
| 21:45 | 4316 | Crusaders Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.81 | 3.58 | 3.58 |
| 21:45 | 4864 | Nottingham vs Burnley | 2.26 | 3.46 | 3.15 |
| 21:45 | 5769 | FC Giugliano 1928 vs Juve Stabia | 2.56 | 3.14 | 2.77 |
| 21:45 | 5790 | Usd Audace Cerignola vs FB Brindisi | 1.51 | 3.93 | 6.50 |
| 22:00 | 1684 | Granada vs Girona | 2.73 | 3.45 | 2.54 |
| 22:00 | 4403 | FC Andorra vs Real Oviedo | 2.18 | 2.96 | 3.40 |
| 22:15 | 1950 | HK Kopavogs vs Fram Reykjavik | 2.20 | 3.82 | 2.60 |
| 22:15 | 2327 | Boavista vs GD Chaves | 1.68 | 3.88 | 4.28 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Septemba 18, 2023
Nipashe



## Felix: Nafurahia maisha mapya hapa Barcelona

UKURASA 21





Picha kushoto ni kiungo mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akiwekwa mtu kati na wachezaji wa Power Dynamos katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Levy Mwanawasa, Zambia na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. Kulia ni beki wa Yanga, Yao Assamoi Kouassi, akiruka kihunzi cha mchezaji wa Al-Merrikh ya Sudan katika mechi ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa Kigali Pele, Rwanda juzi na Yanga kushinda 2-0. **PICHA: WAPIGAPICHA WETU**

# 'SIMBA, YANGA MECHI CAF HAIJAISHA MPAKA IISHE'

### Robertinho, Chama watoa mkakati kiufundi, Jangwani wao wataka rekodi ya...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, akisema kazi kubwa anayoenda kuifanya ni kufanyia kazi sehemu mbili ikiwamo umakini wa safu ya ulinzi na ushambuliaji ili kutafuta nafasi ya kufuzu kucheza makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, watani wao wa jadi, Yanga wamesema msimu huu wamepania kuweka rekodi kwa kuvunja zote zilizowahi kuwekwa na klabu za hapa nchini katika michuano hiyo.

Simba juzi ililazimisha sare ya mabao 2-2 ugenini dhidi ya Power Dynamos ya Zambia katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Levy Mwanawasa nchini humo, wakati Yanga siku hiyo hiyo iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Kigali Pele, Rwanda.

Yanga itarudiana na Al-Merrikh Septemba 30 na kesho yake Oktoba Mosi, mwaka huu, Simba itawakaribisha Power Dynamos, na timu itakayopata matokeo ya jumla kati michezo hiyo inayotarajiwa kupigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, ndiyo itakayotinga hatua ya makundi.

Hivyo, wawakilishi hao wa Tanzania kimataifa hakuna anayeweza kujihakikishia kusonga mbele hadi dakika 90 za pili zitakapomalizika hapa nchini, ingawa Yanga tayari imetanguliza mguu moja ndani kwani sare yoyote ama kutoruhusu kupoteza kwa zaidi ya bao 1-0 itajikatia tiketi.

Kwa Simba inahitaji suluhu, sare ya bao 1-1 ama ushindi ili kusonga mbele, jambo ambalo pia mpaka dakika 90 zitakapomalizika Oktoba Mosi.

INAENDELEA UK. 23

## Singida FG yaikamua Future Shirikisho

**Na Adam Fungamwango**

ELVIS Rupia, mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Kenya msimu uliomalizika, jana alifunga bao pekee lililoipa ushindi wa 1-0 Singida Fountain Gate dhidi ya Future FC ya Misri, katika mechi ya mkondo wa kwanza, Kombe la Shirikisho la Soka Afrika uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Rupia ambaye alikuwa akiichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza akisajiliwa kutoka Polisi ya Kenya, alitumia makosa ya mabeki wa Future kuchelewa kuokoa faulo iliyopigwa na Mourice Chukwu, akaukwamisha kwa shuti la mguu wa kushoto lililompita kipa Mahmoud Genesh kabla ya kujaa wavuni.

Straika huyo aliyefunga mabao 27 kwenye Ligi Kuu ya Kenya na kuvunja rekodi iliyowekwa na Maurice Ochieng aliyefunga mabao 26 mwaka 1976, ameiwezesha Singida kupata ushindi kwenye raundi ya kwanza ya kombe hilo.

Hata hivyo, Singida ambayo inacheza kwa mara ya kwanza michuano ya kimataifa msimu huu, itakuwa na kibarua kizito cha kwenda kulinda ushindi wake huo ugenini zitakaporudiana Oktoba Mosi, Cairo nchini Misri.

Katika mechi hiyo ya jana, dakika ya 17 Bruno Gomez alikaribia kuifungia Singida Fountain Gate bao, lakini mkwaju wake wa faulo uliowababatiza mabeki wa Future na kuwa kona tasa.

Dakika ya 32, Future nusura wapate bao la kuongoza, lakini shuti dhaifu la Bello Babatunde lilidakwa kirahisi na kipa Beno Kakolanya.

Kiungo wa Future, Ali Zazaa akiwatoka mabeki wa Singida na kuingia ndani ya eneo la hatari dakika ya 34, lakini hakuweza kuleta madhara kwa shuti lake hafifi kabla ya dakika mbili baadaye straika Mkenya, Duke Abuya kushindwa kupachika mpira wavuni baada ya shuti kale kali kutoka nje kidogo ya lango.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >